# Mwongozo wa mwalimu

## Wakati wa biblia Kiwango 3 na 4

Msururu A
Masomo 1 - 6

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)

**Misheni yetu**
Kutunga mafundisho ya Biblia kwa walimu ili wafundishe ukweli wa Yesu Kristo kwa kizazi kinachokuja katika dunia yote.

**Vision Statement**
Kufikia kizazi kinachokuja na ufahamu wetu wote katika lugha zao kwa kuendeleza na kusaidia shirika la kimataifa la washiriki waliojitolea.

## HABARI KWA JUMLA

**Kazi inayofanywa na Bible Educational Service:**

Kazi ya mafundisho ya kibiblia (Bible Educational service) inachapisha katika kingereza mafundisho ya Biblia “Bibletime"’, “New Life” na “Gleaner”. Inasaidia vituo vya usambazaji wa mafundisho hii na kila shirika ya namna hiyo inayozitumia katika Uingerezana na pahali pengine duniani, kwa njia ya kuwatembelea, kuwashauri, na wakati wa kuwafundisha. Katika inchi mbalimbali, Bes iliendeleza pia ushirikiano na vikundi nyingi vinavyofanya kazi ya utafsiri, muundo, uchapishaji na usambazaji wa mafundisho. Kila mara inapewa bure kwa wote.

Mafundisho “wakati wa biblia” ilianza pale Irland tangu miaka zaidi ya 50. BES iko na hati miliki ya mafundisho katika kiingereza vilevile katika lugha zote zingine. Sehemu kubwa ya mafundisho hii imechapishwa katika muundo wa A4 na inatumiwa kama mafundisho kwa mfano wa barua katika inchi nyingi zinazozungumza Kiingereza. Kama inajazwa na watoto, masomo inarudishwa, baada ya kila wiki ine, katika kituo kimoja ili ipewe pointi (Bible school Center). Tangu muda mfupi, mafundisho imechapishwa pia katika vitabu vya muundo wa A5, vilivyo na mafundisho ya miezi sita, kupitia Revival Movement katika Irland ya kaskazini. Hii iliwezesha kabisa utumizi wake katika ma kanisa na shule, zaidi katika eneo ambako kazi ya posta haipo tena.

Mafundisho ya BES inapatana pia vema na utumizi wa kibinafsi nyumbani ao katika kundi, ikiwa ndani ya ma kanisa ao ndani ya ma shule. Programu iliyotungwa inawezesha watoto na vijana kuendelea kujifunza Biblia muda wa zaidi ya miaka kumi. Viwango tano vya masomo vinapatikana sasa katika kingereza (miaka 3 - 4, miaka 5 – 7, miaka 8 - 10, miaka 11 – 13, miaka 14 – 16). Kwa kila mmoja wao, programu inachukua miaka tatu. Mtoto ao kijana anaweza kujifunza viwango tofauti kulingana na uwezaji wake kibinafsi. “Wakati wa biblia” inaleta kwa watoto na vijana nafasi kwa kujifunza Neno la Mungu, kujifunza hadisi za Biblia na kuelewa maana ya injili katika maisha yao wenyewe.

Mafundisho inayopatikana katika ufaransa inaweza kuchapishwa kutoka tovu – www.besweb.com – ao kwa kumuomba katibu wa kimataifa. Inapatikana pia kwa lugha zingine katika tovu. Pia kuna vitabu vingine ambavyo vinaweza kuwa vya muhimu kwa inchi mpya ao maeneo inayotaka kuanzisha kituo cha BES.

## Anuani ya kufaa:

**UK (Northern Ireland) Office (ghala za masomo zote)**
Bw. Samuel Balmer
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Phone: 0286 632 2462

Site web: www.besweb.com
Email: info@besweb.com

## MWONGOZO WA MWALIMU

Katika mwanzo, mafundisho ya “Wakati wa Biblia” ilitolewa kwa mfano wa mafundisho kwa njia za barua kwa ushirikiano na kituo kimoja cha “shule ya Biblia kwa njia ya posta”. Lakini, zaidi na zaidi mafundisho hii inasomwa pahali ambapo kazi ya posta siyo ya kuaminika, hasa katika shule na ma kanisa katika Afrika, India na pahali pengine. Mwongozo wa mwalimu uko pale kwa kusaidia wale wanaotumia mafundisho katika mazingiza kama haya. Kitabu hiki kinatungwa juu ya kuwa mwongozo wa kiwango 3 na 4, ambavyo vinakusudiwa watoto kutoka umri wa miaka 11 hadi 16.

Maelezo ya mwongozo huu yanafuata maandiko ya Biblia ambayo ni namna moja na ile iliyo katika mafundisho yenyewe. Mafundisho, na maelezo, imetungwa mu namna ya somo moja kwa wiki. Kwa hiyo, masomo katika Aprili inaambatana na Pasaka na masomo katika Desemba inaambatana na Krismasi.

Kulingana na pahali, ao masomo kwa wiki katika muundo wa A4, ao vitabu vya muundo wa A5 ambamo muna masomo 24 kwa miezi 6, vitatumiwa. Ni mwalimu ndiye atagawa masomo A4 kwa mwezi. Kila wiki kartasi itajazwa kwenye kanisa ao shule, ao itapelekwa kwa mtoto na kurudishwa yenye kujazwa, baada ya wiki moja. Mwisho wa kila mwezi, mwalimu atachukua masomo na ataipatia ma pointi; atairudisha kwa wanafunzi yenye kurekebisha, kwa haraka iwezekanayo.

Kitu kizuri ni kwamba, vitabu vya muundo wa A5 vinapaswa kuchukuliwa na kupewa ma pointi mwisho wa kila mkutano, lakini mara nyingi tunaona kwamba haiwezekane. Katika kesi hii, ni vema kuigawa kwa wanafunzi wengine, na mwalimu ataleta ma pointi kwa masomo akisema kwa sauti na wakati wanafunzi watakuwa wanarekebisha na kuweka alama katika masomo ya wenzao. Katika ukurasa wa mwisho wa kila kitabu, kuna pahali ambapo inaruhusu kuandika kiwango cha kufaulu cha kila mwezi, na pia maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Kwenye cheti hiki inaonekana nambari ya kiwango cha kufaulu kwa mwanafunzi muda wa miezi sita ya masomo.

## MASHAURI YA MUHIMU KWA WALIMU

Hapa, lengo siyo kwamba ni maagizo kwa walimu na kuwanyima uwezekano wote wa kulinganisha somo, kufuatana na mawazo na mipango yao wenyewe. Ni mapendekezo tu ambayo inaweza kusaidia katika utumizi wa mafundisho ya “wakati wa Biblia”.

- **Kujua historia vizuri –** Mwalimu anapaswa kufanya yote iwezekanayo ili ajue vizuri historia ya Biblia, vilevile mafundisho ya “wakati wa Biblia” ambayo inaambatana nayo. Iliyo vema ni kwamba amalize yeye mwenyewe kujifunza somo kabla ya kuwaambia watoto. Maelezo ya mwongozo inapaswa pia kusomwa na uangalifu kwa kusaidia katika kupangwa kwa kila somo.
- **Kuelewa mafundisho ya kushika –** Juu ya kila ukurasa, unaweza kusoma: “tunajifunza kwamba”, inafuatiwa na nukta mbili kubwa ambayo tunatumaini kwamba watoto wataelewa kisha kusikia maelezo ya mwalimu na kisha kujifunza mafundisho ya “wakati wa biblia”. Nukta kubwa ya kwanza inaelekea ufahamu na uelewa wa historia. Ya pili inatia watoto moyo kwa kushika kibinafsi mafundisho inayopatikana katika historia hiyo. Ma nukta kubwa hii ya kushika inafanya muhtasari wa ukweli muhimu ambao ulifundishwa katika somo. Mwalimu anaweza kuitumia kwa “kujipima kibinafsi” kutokana na mafundisho iliyopewa, pia uelewa wa watoto.
- **Kutanguliza –** Mafundisho yote inaanza kwa kuambatanishwa na mambo ambayo watoto wenyewe waliishi, inayofanana na jambo ambayo inaelezwa katika historia. Mawazo mengi yamependekezwa juu ya kutanguliza hadisi na kuwezesha watoto wajifunze kwa bidii tangu mwanzo wa huu wakati wa mafundisho ya Biblia.
- **Kufundisha –** Ma nukta kubwa za historia zimetajwa. Tunatumaini kwamba mwalimu hatakuwa anaisoma wakati anaieleza. Lakini, lazima ajue vizuri historia ili aweze kuisema kwa bidii na kuamsha akili. Atafanya kwamba wanafunzi waelewe mafundisho kubwa ya kushika na atawaongoza katika jinsi wanaweza kujibu na kuitumia. Tulijaribu, ilivyowezekana mara kwa mara kutoa maelezo fulani wakati historia inapoelezwa. Hiyo inaonekana kila mara katika maandishi ya *italiki*.
- **Kujifunza –** Kila historia inaambatana na shairi muhimu. Wakati mwingine kuna mbili, kama ya pili iliongezwa, inaweza kuwa mwepesi kukamata katika akili. Tunatumaini kwamba watoto watajifunza vizuri ma shairi muhimu na mara kwa mara watakuwa na nafasi kwa kuirudia juu ya kuikumbuka vema.
- **Kujaza somo –** Ikiwa masomo inafundishwa katika shule, mwalimu atajua kama watoto wanaweza kujaza masomo pekee ao kama wanahitaji kusaidiwa. Ikiwa ni lazima, inapaswa mwalimu awasomee maandiko ya

somo watoto wengine ambao hawataweza kusoma pekee. Katika kesi moja kama katika nyingine, inaweza kuwa ya mafaa kuamsha akili ya wanafunzi katika ma nukta moja ambayo inapatana na maswali.

Kama mafundisho ya “wakati wa biblia” inatumiwa katika mazingira ingine isiyokuwa shule, ni ya muhimu kwamba mwalimu awe mwema na tayari kusaidia watoto ili mafundisho hii isionekane kuwa kitu cha magumu na cha kuchokesha, lakini kwa tofauti ionekane kuwa wakati wa kufurahisha. Ni ya muhimu pia kuwatia moyo watoto na kuwapongeza wakati wanapojifunza.

- **Kuimarisha** – Mawazo ya kibinafsi ao katika kundi, michezo kidogo imetungwa kwa ajili ya kusaidia majifunzo na marudio ya historia.
- **Kushika –** Katika sehemu hii, changamoto ya kibinafsi imepewa kwa wanafunzi. Mara nyingi, kazi inapewa kwa ajili ya kuongoza wanafunzi kuambatanisha mafundisho na maisha yao ya kila siku.
- **Kuonyesha –** Katika ma kesi nyingine, tunajua kwamba inaweza kuwa magumu kuwa na vyombo vya kuonyesha picha. Lakini ikiwezekana, ni ya muhimu sana kuonyesha picha ao vitu ambavyo vitasaidia watoto kuelewa historia kwa njia ya mifano. Ma picha inaweza kupakuliwa katika tovu www.freebibleimage.org. Eikon Bible Art (www.eikonbibleart.com) inaleta pia vyombo vya kuonyesha picha lakini vifaa vyake ni vya kuuza. Ikiwezekana, mifano iliyo katika mafundisho ya “wakati wa biblia” inaweza kunenepeshwa na fotokopi, kisha kuwekwa rangi na kutumiwa kwa kuonyesha picha.

## Kufundisha mstari muhimu

1) Shairi inaweza kuandikwa katika karatasi kubwa ao katika kibao. Kisha, maneno mengi inaweza kuondoshwa polepole wakati watoto wanatamka shairi, mpaka wakati hakutabaki tena neno hata moja na wafikie kutamka shairi yote mzima, bila kusaidiwa.
2) Kwa kutanguliza mstari muhimu unaweza kutumia:
   a) Mchezo wa kujaza visanduku: Mstari muhimu inaandikwa na herufi nyingi ambazo zinakosekana, hakuna neno inayo herufi zote. Watoto wanapendekeza herufi juu ya kujaza ma tundu, mpaka wakati mmoja wao anatambua shairi.
   b) Kila mtoto ana Biblia na wote wanafukuzia ili wavumbue shairi wa kwanza. Wa kwanza kuipata lazima aisome kwa sauti kubwa.

## Kusimamia muda

- Maelezo yote yameundwa namna moja, ikilinda taratibu moja ya sehemu tofauti. Lakini ikiwa ya lazima, mwalimu anaweza kubadilisha muundo.
    1. Kueleza na kufundisha historia: Karibu dakika 15,
    2. Kujifunza Mstari muhimu: karibu dakika 5 mpaka 10,
    3. Kujaza karatasi: dakika 20,
    4. Michezo na ma kazi nyingine: dakika 5 mpaka 10.

Kumbuka haya:

“Uniambie na naweza kusahau,<br>Unionyeshe na nitakumbuka,<br>Unishirikishe na nitaelewa”

## Kitabu cha Wakati wa Biblia

| | Hatua ya 1 (miaka 5-7)<br>Hatua ya 2 (miaka 8-10) | Hatua 3 (miaka 11-13) | Hatua 4 (miaka 14+) |
|---|---|---|---|
| MSURURU A | 1. Uumbaji<br>2. Noa<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Abrahamu<br>6. Abrahamu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa kwanza<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas | 1. Uumbaji<br>2. Noa<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Petro<br>6. Abrahamu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas | 1. Uumbaji na kuanguka<br>2. Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro/Msalaba<br>5. Petro<br>6. Abrahamu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya kikristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Historia ya Krismas |
| MSURURU B | 1. Utoto wa Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Msalaba<br>5. Mafumbo<br>6. Yosefu<br>7. Yosefu<br>8. Yesu anakutana na watu<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Historia ya Krismas | 1. Mafumbo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yosefu<br>7. Yosefu<br>8. Waandishi wa Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Historia ya Krismas | 1. Mafumbo<br>2. Miujiza<br>3. Betania<br>4. Bwana Yesu<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Maisha ya Yosefu<br>8. Njia ya kwenda<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Sheria<br>12. Muujiza wa Krismas |
| MSURURU C | 1. Danieli<br>2. Miujiza ingine<br>3. Miujiza ingine<br>4. Historia ya pasaka<br>5. Ruta na Esiteri<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Historia ya Krismas | 1. Danieli<br>2. Miujiza ingine<br>3. Miujiza ingine<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruta<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu waliotumiwa na Mungu<br>12. Historia ya Krismas | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Yesu ine<br>3. Nguvu ya Bwana<br>4. Bwana Yesu<br>5. Ruta<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yosua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu wa Agano la Kale<br>12. Kuzaliwa kwa Kristo |

| | A1 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Katika Mwanzo<br>Kichwa – Mungu anaumba dunia | A1 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Uumbaji<br>Kichwa – Katika mwanzo |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 1:1-19***<br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 1:1***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu aliumba dunia na vyote vilivyomo.<br>2. Mungu alifanya kila mtu duniani, anapenda na kujua kila mtu kibinafsi. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 1:1- 31***<br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 1:10; Isaya 45:18***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu aliumba dunia.<br>2. Mungu ni mwenye nguvu yote.<br>3. Mungu alifanya mtu kwa mfano wake. |
| **KUTANGULIZA** | Ambia kila mwanafunzi aandike jibu moja ya maswali hii. Imeruhusiwa kuwazia! Kisha kila mtu atasema majibu yake kwa mwanafunzi mwingine.<br><br>Baada ya dakika kidogo, leta majibu ifwatayo:<br>1. Kulingana na shirika la anga la ulaya, ni magumu kusema kuna nyota ngapi. Wanawaza kwamba wingi wa nyota ni milioni elfu mia moja katika anga yetu moja tu. Na kuna ma milioni na ma milioni za anga zingine! Ile inafanya nyota nyingi!<br>2. Kulingana na hesabu ya sasa, katika dunia kuna watu karibu bilioni 7 duniani. | Zungumzeni pamoja kuhusu maswali ifuatayo, mbele wawili kwa kundi kisha katika kundi kubwa:<br>1. Ni wakati gani ulifanya tendo lako la mwisho katika kuumba?<br>2. Ulipendezwa na matokeo? |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu alikuwako, kabla ya kuwepo kwa kitu chochote.<br>2. Mungu alifanya dunia muda wa masiku sita.<br>3. Siku ya 1: Mungu anaumba nuru na anaitenganisha na giza; Siku ya 2: Mungu anafanya mbingu na anaitenganisha na maji iliyo chini; Siku ya 3: Mungu anakusanya maji na anaita inchi kavu “dunia”. Dunia inazaa majani na miti. Siku ya 4: Mungu anaweka mianga katika anga: Jua, mwezi na nyota; Siku ya 5: Mungu anaumba viumbe baharini na ndege; Siku ya 6: Mungu anaumba Wanyama.<br>4. Kisha, Mungu anaumba mtu kwa mfano wake, mwanaume na mwanamke, juu ya kujaza na kutawala dunia pia viumbe vyake.<br>5. Mungu analeta chakula kwa watu na kwa viumbe vyake vyote.<br>6. Mungu anaangalia vyote ambavyo alifanya na anawaza kwamba ni vizuri sana!<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu aliumba dunia kwa siku sita.<br>2. Siku ya 1: Mungu anaumba nuru na anaitenganisha na giza: Siku ya 2: Mungu anafanya mbingu na anaitenganisha na maji iliyo chini; Siku ya 3: Mungu anakusanya maji na anaita inchi kavu “dunia”. Dunia inazaa majani na miti. Siku ya 4: Mungu anaweka mianga katika anga: Jua, mwezi na nyota; Siku ya 5: Mungu anaumba viumbe baharini na ndege; Siku ya 6: Mungu anaumba Wanyama.<br>3. Uwezo wa Mungu ni wa ajabu: Anaumba dunia kwa neno lake, na anaifanya kwa siku sita tu!<br>4. Mungu anafanya wanadamu kwa mfano wake; anawaumba mwanaume na mwanamke.<br>5. Wakati Mungu anaangalia yote ambayo alifanya, uamzi wake ni kwamba vyote ni vizuri sana.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| **KUIMARISHA** | Katika ma kundi za watu ine, fanya kibao moja kwa kuonyesha kila moja ya ma siku sita za kuumba kwa Mungu | Unajifunza nini katika hii mafundisho kuhusu tabia ya Mungu? Kuhusu hii, ndika shairi kidogo wa aya. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Mungu ni mwenye nguvu yote na aliumba kila kitu. Ingawa viumbe vyake ni vingi kabisa, Mungu alifanya kila mmoja wetu, anatujua na anatupenda. Ile inapaswa kuonyesha namna gani hali yetu mbele ya Mungu na viumbe vyake? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Mungu aliumba dunia yetu na alituumba pia. Namna gani inaweza hii inaweza kubadilisha Maisha yetu?<br>2. Soma ***Mwanzo 1:26-27*** na ***Isaya 45:18***. Mungu alikuwa na Mawazo gani juu ya mtu? Hii inafanya tendo gani katika namna yetu ya kuishi leo? |

| | A1 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Katika Mwanzo<br>Kichwa – Mungu anaumba mtu | A1 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Uumbaji<br>Kichwa – Unamalizika |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 1:20:31***<br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 1:27***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu aliumba wanyama, lakini aliumba mtu aliye tofauti nao.<br>2. Mungu aliumba mtu kwa mfano wake, ili afanane naye pia atawale viumbe.<br>3. Mungu alifanya watu ili wawe katika mapatano naye pia wamoja na wengine.<br>4. Mungu alimfanya mtu kuwa mwenye madaraka. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 1:1- 31***<br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 1:10; Isaya 45:18***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu alipumzika siku ya saba.<br>2. Mungu alifanya sabato kwa ajili ya kupumzika.<br>3. Mungu alileta uhai kwa mtu.<br>4. Uzima wa mtu una bei ya kipekee. |
| **KUTANGULIZA** | Fanyeni mchezo wa “pictionary”, kuvumbua majina ya wanyama kwa kutazama picha zao. Gawanya darasa mu ma kundi ya watu 4. Leta karatasi kwa kila kundi, kibao ao kalamu ya wino. Memba moja wa kundi anapaswa kuchora nyama moja na wengine wanapaswa kuvumbua ni nyama gani. | Maongezi ya kusimama. Tayarisha ma karatasi kidogo yenye kuandikwa “ndivyo”, “sivyo” na “kutokuwa na uhakika” juu ya kuonyesha “nafasi” tatu katika chumba hiki. Soma maelezo ifuatayo uwaambie watoto waende kwenye nafasi ambayo inaonyesha mawazo yao kuhusu kila moja.<br>• Jinsi siku ya jumapili iko ya kipekee, haiku na maana leo.<br>• Siku ya jumapili ni wakati mzuri kwa kujifunza nyumbani na kununua vitu.<br>• Ni vema kukataza michezo mu siku ya jumapili.<br>• Utafiti wa mayai ya kibinadamu unakubaliwa.<br>• Waamini hawapaswi kujiingiza katika ma vita. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu aliumba Wanyama ili wazae na kuongezeka.<br>2. Mungu aliumba mtu kwa mfano wake, ili afanane naye, pia atawale Samaki, wa ndege na Wanyama.<br>3. Mungu aliumba mtu, wanadamu, mwanaume na mwanamke.<br>4. Mungu alibariki mwanaume na mwanamke na aliwapa kazi na mapashwa (wanapaswa kuzaa na kuzidi, kujaza dunia, kuiongoza, na kutawala viumbe vya Mungu.<br>5. Mungu alileta msaada wa chakula, kila kitu ambacho tunahitaji kwa kuishi.<br>6. Mungu alipendezwa na kila kitu ambacho aliumba. Alisema kwamba ni vema sana!<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Katika mwanzo, Mungu alikuwako, kabla ya kitu chochote. Neno (Bwana Yesu) ni Mungu na alikuwa Pamoja na Mungu katika mwanzo. Aliumba kila kitu ambacho kilifanyika; hakuna kitu ambacho kilifanyika pasipo yeye. Mungu ndiye muumbaji na ni Mungu wa mianzo<br>2. Mungu aliweka mtu katika shamba la Edeni.<br>3. Mungu aliweka pia miti mbili ya kipekee kabisa katika shamba la Edeni: mti wa uzima na mti wa kujua uzuri na ubaya.<br>4. Mungu alipumzika siku ya saba na aliweka siku ya kipekee ya mapumziko kwa mwanadamu.<br>5. Mungu alimpulizia mtu pumzi ya uzima. Kwa hiyo wanadamu weko tofauti na wanyama. Uzima wa mwanadamu ni wa kipekee na una bei ya kipekee.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| **KUIMARISHA** | Zungumzeni pamoja katika ma kundi kidogo kihusu ma nukta ifuatayo, kisha mueleze majibu yenu mbele ya kundi lote:<br>• Mungu aliumba wanadamu kwa mfano wake ili watawale juu ya samaki, wa ndege na wanyama. Sasa tunapaswa kuwatendea namna gani?<br>• Mungu alitaka kwamba tuwe katika uhusiano naye pia wamoja na wengine. Namna gani tunaweza kuonyesha mapendo kwa Mungu na kwa watu wengine: 1) nyumbani, 2) shuleni, 3) kanisani. | Zungumzeni pamoja katika ma kundi kidogo kuhusu ma nukta ifuatayo, kisha mueleze majibu yenu mbele ya kundi lote:<br>• Soma ***Kutoka 20:8*** na ***Marko 2:27***. Ma shairi hii ina umuhimu gani kwetu leo?<br>• Tunajifunza kwamba uzima wa mwanadamu una bei ya kipekee. Namna gani ukweli huu unaweza kuongoza uamuzi tunaofanya katika mambo kama sayansi, afia, sheria na utunzaji wa wazee? |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Mungu alituumba ili tuwe katika uhusiano na yeye pia na watu wengine. Kuna tofauti gani katika Maisha yetu ya kila siku ikiwa tunatubu na kutia tumaini yetu ndani yake?<br>2. Tuombe ili Mungu atusaidie kutimiza mapashwa yetu pia tuonyeshe tabia yake (kwa mfano, mapendo yake, wema wake, haki yake) wiki hii katika familia yetu, shuleni mwetu, pia kundi letu kanisani. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Namna gani tunatia katika tendo (ao hatutie katika tendo) mapumziko ya mu siku ya jumapili (sabato) katika Maisha yetu leo mapumziko ya mu siku ya jumapili ni ya muhimu? Kwa sababu ya nini?<br>2. Tutafanya je ili maisha yetu ionyeshe kwamba tunaamini kwamba uzima wa wanadamu umepewa na Mungu pia una bei ya kipekee? |

| | A1 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Katika Mwanzo<br>Kichwa – Vitu vinaharibika! | A1 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Uumbaji<br>Kichwa – Kuonekana kwa zambi |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 2:15-17; 3:1-13***<br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 3:3***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Adamu na Eva wanakosa kumtii Mungu.<br>2. Adamu na Eva wanaona haya na wanapaswa kupata matokeo ya zambi yao. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 2:15-20; 3:1-7***<br>**Mstari muhimu:** ***Waroma 3:23; 6:23***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anamuamuru mtu asikule matunda ya mti wa kujua uzuri na ubaya.<br>2. Nyoka anadanganya Eva na Adamu na wanakosa kutii amri ya Mungu.<br>3. Adamu na Eva wanaona haya. |
| **KUTANGULIZA** | Uliza kundi kama kuna ma kanuzi ya kushika shuleni mwao. Kwa nini ni ya muhimu? Nini inaweza kufika ikiwa haziheshimiwe? | Uwaambie wanafunzi wazungumzie pamoja wawili wawili kuhusu mambo ifuatayo:<br>• Mapashwa ambayo wanaweza kuwa nayo shuleni/kazini / nyumbani.<br>• Ma kanuni ao maagizo ambayo wanapaswa kufuata.<br>• Nini inaweza kufika ikiwa ma kanuni hizi haziheshimiwe, ikiwa hazishikwe? |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anaweka mtu katika shamba la Edeni na anamwambia aitunze. Mungu anampa mwanadamu kila kitu anachohitaji, lakini kuna kanuni moja ambayo mtu anapaswa kushika. Haruhusiwe kula tunda la mti unaitwa “mti wa kujua uzuri na ubaya”. Mungu anaonya kwamba mtu atakayeikula, atakufa.<br>2. Kisha, Mungu anampa mtu kazi ya kuleta ma jina kwa wanyama na wa ndege.<br>3. Mungu anaumba mwanamke kwa ajili ya kumsaidia mwanaume atimize mapashwa yake. Katika ndoa, mwanaume na mwanamke wanafanya familia mpya na wanatumika pamoja, kama timu.<br>4. Yule nyoka mwenye hila, adui wa Mungu mwenye kujigeuza, analeta shaka kuhusu amri ya Mungu. Anawaambia Adamu na Eva kwamba hawatakufa kama wanakosa kutii agizo hii. Adui anadanganya mwanamke naye anakula tunda ambayo Mungu aliagiza wasikule. Anampa mume naye anakula pia.<br>5. Wakati mume na mke walipofanya vile, wanajisikia kuwa wenye ole. Wanatengeza majani ya mukuyu ili wajifunike, na wanajificha katika miti. Mungu anawaita na wanamuonyesha mambo ambayo walifanya. Adamu anasema kwamba ni kosa la Eva na Eva kwamba ni kosa la nyoka.<br>6. Mungu analaani nyoka. Adamu na Eva wanapaswa kuishi matokeo ya zambi yao. Wanapata maumivu na wanapaswa kushindana na kutumika nguvu. Maisha inakuwa magumu, na siku moja itabidi wa kufe.<br>7. Mungu anafanyia Adamu na Eva mavazi ya ngozi ya nyama, na anawafukuza katika shamba la edeni ili awaweke mbali na mti wa uzima.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anampa Adamu kazi ya kutunza shamba na ua kuleta ma jina kwa wa ndege na wanyama.<br>2. Mungu anasema kwamba mtu anaweza kula ma tunda ya miti yote ila tu moja: Tunda la mti wa kujua uzuri na ubaya. Mungu anamuonya kwamba matokeo ya kula tunda la mti huu itakuwa hakika kufa.<br>3. Mungu anaumba msaidizi kwa ajili ya mwanaume, anayeitwa mwanamke. Wanapaswa kutumika pamoja. Katika ndoa, mwanaume na mwanamke wanafanya familia mpya na wanatumika pamoja, kama timu.<br>4. Yule nyoka mwenye hila anamdanganya Eva na anakosa kumtii Mungu , anakula tunda iliyokatazwa na anampa pia mwanaume anakula. Kwa kula tunda, mwanaume pia anakosa kumtii Mungu. Adamu na Eva wanashindwa kufikia agizo kamilifu ya Mungu kwa sababu walikula tunda ile.<br>5. Adamu na Eva wanajua kwamba walikosa kumtii Mungu na wanaona haya kwa ile. Wanapaswa kuishi matokeo ya kukosa kutii amri ya Mungu.<br>6. Wanapaswa kupata azabu ya Mungu.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| **KUIMARISHA** | Ambatanisha somo hii na ***Waroma 5:12***. Tangu Adamu na Eva walikosa kutii, sisi wote tunazaliwa wenye zambi. Ambia wanafunzi walete mifano ya kukosa kutii amri za Mungu katika maisha yetu ya kila siku. Ina matokeo gani 1) kwetu 2) kwa watu wengine? | Ni matokeo gani ilikuwa ya kukosa kutii kwa Adamu na Eva? Soma ***Waroma 5:12-14*** na ***18-19***. Namna gani kukosa kutii kwa Adamu kunatugusa sisi leo? |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Tunapaswa kutubu mbele ya Mungu ili atusamehe na aturudishe upya. Sasa tutaweza kuishi kwa ajili yake na kufuata amri zake. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Kwetu sisi waamini, kwa nini ni ya muhimu kumtii Mungu?<br>2. Katika kutenda, tunaweza kumtii Mungu namna gani katika Maisha yetu ya kila siku? |

| | **A1 – KIWANGO 3**<br>**Somo 4 – Katika Mwanzo**<br>**Kichwa – Kutenda jinsi Mungu anataka!** | **A1 – KIWANGO 4**<br>**Majifunzo 4 – Uumbaji**<br>**Kichwa – Matokeo ya zambi** |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 4:1-16***<br>**Mstari muhimu:** ***Yoane 14:6***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Abeli anafuata njia ya Mungu lakini Kaina anafuata njia yake mwenyewe. Mungu anakubali sadaka ya Abeli lakini anakataa ile ya Kaina.<br>2. Kaina anamuua Abeli. Mungu anamfukuza katika inchi na anamfanya kuwa mtu wa kutangatanga. Kaina anaondoshwa katika uwepo wa Bwana.<br>3. Kuna njia moja tu inayopeleka kwa Mungu, na ni njia yake yeye! | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 3:7-24***<br>**Mstari muhimu:** ***1 Wakorinto 15:22; Waroma 3:23; 6:23***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Adamu na Eva wanajaribu kujificha kwa Mungu.<br>2. Mungu analaani nyoka ambaye aliwadanganya.<br>3. Mungu anawaambia Adamu na Eva kwamba watapata maumivu na mateso kwa sababu ya zambi yao.<br>4. Mungu analeta mavazi kwa ajili ya kufunika uchi wa Adamu na Eva.<br>5. Mungu anawafukuza Adamu na Eva kutoka katika shamba la Edeni. |
| **KUTANGULIZA** | Ni nini itafika ikiwa unaenda katika safari bila kuangalia anuani ao maelezo kuhusu njia ya kufuata? Imekwisha kukufikia kwamba unaacha kufuata maelezo na unapotea? Kaina hajali kamwe maagizo ya Mungu na mwisho wake anakuwa mpotevu wa kutangatanga. | Ambia watoto wakumbuke mambo moja ya utoto wao wakati walikosa kutii, nyumbani ao shuleni. Walijisikia namna gani? |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Adamu na Eva weko na wana wawili. Abeli anakuwa mchungaji na Kaina mlimaji wa shamba.<br>2. Mungu anakubali sadaka ya nyama ambayo Abeli analeta: Mwana kondoo mzuri zaidi ya wazaliwa wa kwanza wa kondoo zake. Mungu anakataa sadaka ya Kaina: sehemu ya mavuno yake. Kaina anakasirika na anajisikia kuwa amechoka.<br>3. Mungu anamuonya Abeli kuhusu zambi na anaonyesha umuhimu wa kufuata njia mzuri, ile ya Mungu. Kaina hataki kutubu, na hataki kusikia ile Mungu anamwambia.<br>4. Kaina anamuua Abeli, ndugu yake. Mungu anamfukuza inje inchi, na anakuwa mkimbizi wa kutangatanga, inje ya uwepo wa Mungu.<br>5. Abeli alielewa kwamba alihitaji kutoa mwana kondoo kwa Mungu. Lakini Kaina hasikuwe kwa Mungu kulingana na njia ya Mungu, na aliazibiwa.<br>6. Sadaka ya Abeli ni mfano wa zabihu ambayo Bwana Yesu atatimiza katika msalaba.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Kukosa kutii kwa Adamu na Eva kuliwafanya wanajua uzuri na ubaya, pia uchi wao. Wanaogopa na wanataka kujificha mbele ya Mungu.<br>2. Mungu anawauliza ma swali Adamu na Eva. Anataka kwamba waitike ubaya ambao walifanya. Lakini wote wawili wanashitaki mwingine.<br>3. Adamu na Eva wanapaswa kuishi matokeo ya kukosa kutii kwao: wanapata maumivu, wanapaswa kujikaza ili waishi, na wanafukuzwa inje ya uwepo wa Mungu katika shamba la Edeni.<br>4. *Sisi pia tunapaswa kuishi matokeo ya zambi yao: Kwa sababu Adamu alifanya zambi, tunakuwa kama yeye na tutakufa sisi wote.*<br>5. Mungu ndiye mwenye neema nyingi kabisa. Anawapa Adamu na Eva mavazi ya Ngozi ya nyama ili wafunike uchi wao. Waroma 6:23 inatufundisha kwamba Mungu analeta zawadi ya bure ya usima wa milele kwa njia ya Bwana Yesu Kristo, ikiwa tunampokea kama Mwokozi wetu.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| **KUIMARISHA** | Katika mstari muhimu huu, Yesu anasema kwamba yeye ndiye njia moja tu inayopeleka kwa Mungu. Kwa njia gani zingine watu wanajaribu kumpendeza Mungu?<br>Chora picha moja, na uandike juu yake huu msatri muhimu. | Tunajifunza nini kuhusu tabia ya Mungu kupitia majifunzo hii?<br>Ambatanisha majifunzo hii na ***Waroma 5:12***. Tangu kukosa kutii kwa Adamu na Eva, sisi wote tunazaliwa wenye zambi. Ambia wanafunzi walete mifano ya kukosa kutii amri za Mungu katika Maisha yetu ya kila siku. Matokeo yake ni nini 1) kwetu na 2) kwa wengine? |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Ujifunze kushika katika akili ile mstari muhimu.<br>2. Unamfuata Yesu, njia moja tu inayoelekea kwa Mungu. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Ombeni Mungu awapatie nguvu kwa ajili ya kumtii na mumshukuru kwa kuwa, kwa neema yake, alitayarisha yote kwa ajili ya nyakati ile tunamkatisha tamaa na kumuhuzunisha<br>2. Tunapaswa kutubu mbele ya Mungu ili atusamehe na kutufanya upya. Sasa tutaweza kuishi kwa ajili ya kumpendeza na kufuata amri zake. |

| | A2 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Noa na garika<br>Kichwa – Kujengwa kwa Safina | A2 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Kaina na Abeli<br>Kichwa – Kuabudu Mungu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 6:5-22***<br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 6:8***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu ni mtakatifu. Zambi ya watu inavunja moyo wa Mungu.<br>2. Mungu anaamua kumuokoa Noa. Mungu anamwambia Noa kujenga Safina ili amuokoe, yeye, familia yake na wanyama wawili na ndege wa kila aina.<br>3. Noa anafanya kabisa kile Mungu alimwambia afanye. Noa anamtumainia Mungu na anamtii. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 4:1-16***<br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 11:4***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Abeli anakuja kwa Mungu mu namna ambayo Mungu anataka. Mungu anakubali sadaka ya Abeli.<br>2. Kaina anakuja kwa Mungu mu namna yake mwenyewe. Mungu anakataa sadaka ya Kaina. |
| KUTANGULIZA | Onyesha kundi ma kanuni ambayo imepewa juu ya kufanya mchezo ao namna ya kufanya mkate. Zungumzeni pamoja nao kuhusu umuhimu wa kufuata maagizo wakati wa kufanya ao kutengeneza kitu fulani. Fasilia kwamba Mungu alimpa Noa maagizo kamili na kwamba Noa aliishika kabisa. | Fanya daftari ya mambo ambayo inalazimisha kufuata maagizo. Ni nini inafika wakati hatuifuate? |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Katika dunia yote watu wanakuwa waovu kabisa wabaya sana. Zambi zao na kukosa kutii kwao kunamuhuzunisha Mungu kabisa.<br>2. Mungu anaamua kuharibu wanadamu wote na Wanyama ambao aliumba.<br>3. Noa eko tofauti. Anampendeza Mungu. Yeye ni tofauti na wengine wote kwa sababu anafanya mambo ya haki, pia kwa sababu anampenda Mungu na anamtii.<br>4. Mungu anamuonya Noa kwamba ataharibu kwa njia ya garika, wanadamu wote pia viumbe vingine vilivyo na uhai, kwa sababu wamejaza dunia na jeuri.<br>5. Mungu anampa Noa maagizo kamili kwa ajili ya matayarisho yote. Anamuonyesha Noa jinsi ya kujenga Safina kubwa kwa ajili ya kumuokoa, yeye, familia yake pia wawili wa kila aina ya viumbe vilivyo hai.<br>6. Noa anamtumainia Mungu na anafuata maagizo yake kabisa.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Adamu na Eva weko na wana wawili. Abeli ni mchunga kondoo na Kaina ni mlimaji.<br>2. Mungu anakubali sadaka ya nyama ambayo Abeli analeta: Mwana kondoo mzuri zaidi ya wazaliwa wa kwanza wa kondoo zake. Mungu anakataa sadaka ya Kaina: Mimea ambayo aliotesha. Kaina anakasirika na anakata tamaa.<br>3. Mungu anamuonya juu ya zambi na anamufasilia umuhimu wa kutenda kulingana na mapenzi ya Mungu. Kaina hauzunike hata mara moja juu ya mambo ambayo alifanya. Hamusikie Mungu.<br>4. Kaina anamuua Abeli, ndugu yake. Mungu anamfukuza inje ya inchi, na anakuwa mtu wa kutangatanga mbali, inje ya uwepo wa Mungu.<br>5. Abeli alielewa kwamba alihitaji kutoa mwana kondoo kwa Mungu. Lakini Kaina hasikuwe kwa Mungu kulingana na jinsi Mungu alitaka, na aliazibiwa.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| KUIMARISHA | Rudieni historia hii kwa njia ya maswali inayoambatana na vitu ambavyo tunajifunza katika somo hii kuhusu Noa, familia yake na maangizo ambayo Mungu alimpa. | Someni mstari muhimu, ***Waebrania 11:4***. Shairi hii inafanya namna gani muhtasari wa tofauti iliyo kati ya Abeli na Kaina? |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Noa alimwamini Mungu na alifanya kabisa jinsi Mungu alimwambia. Tunaweza kumwamini Mungu namna gani? Unamwamini? Noa alimwamini Mungu na Mungu alimuokoa. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Tunajifunza nini katika Maisha na matendo ya Abeli na Kaina?<br>2. Tutatia namna gani mafundisho hii katika tendo ndani ya maisha yetu ya leo? |

| | **A2 – KIWANGO 3**<br>**Somo 2 – Noa na garika**<br>**Kichwa – Ndani ya Safina** | **A2 – KIWANGO 4**<br>**Majifunzo 2 – Enoka na Noa**<br>**Kichwa – Kutembea na Mungu** |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 7:1-20***<br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 7:5***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu alitengeneza njia ya kumuokoa Noa na familia yake.<br>2. Noa anamwamini Mungu na anafanya kabisa jinsi Mungu anamwambia afanye. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 5:21-32***<br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 11:5***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Enoka na mjukuu wake, Noa wanaishi katika ushirika kabisa na Mungu.<br>2. Hawa watu wawili weko tofauti na wengine katika uhusiano wao na Mungu. |
| **KUTANGULIZA** | Umekwisha kufanya safari Pamoja na familia yako? Mulijitayarisha namna gani? | Kuishi katika uhusiano na Mungu inapaswa kututofautisha na watu wengi! Jinsi gani wakristo wanapaswa kuwa tofauti na watu wengine? Angalia daftari hii ya ma tabia. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anamuonya Noa kwamba baada ya siku saba atatuma garika.<br>2. Mungu anamwambia Noa aingie pamoja na Wanyama ndani ya Safina ili waweze kuishi baada ya garika.<br>3. Siku ile, na umri wa miaka 600, siku ya makumi saba ya mwezi wa 2, Noa anachukua familia yake na Wanyama, kama vile Mungu alimwambia, na anawaingiza wote ndani ya Safina. Garika inafika baada ya siku saba, kama vile Mungu alivyosema.<br>4. Mungu anafunga mlango wa Safina wakati Noa, mke wake na wanyama wanaingia, anawalinda salama ndani ya Safina. Pekee yao Noa, familia yake na wanyama ndani ya Safina, wanaishi baada ya garika kubwa. Mvua inanyesha muda wa siku 40! Maji inapanda zaidi ya mita 7 juu ya milima mrefu sana.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Enoka anaishi mpaka miaka 365 katika ushirika na Mungu.<br>2. Biblia inasema kwamba Enoka hakufa kama wanadamu wengine. Mwisho wa Maisha yake, anatoweka, kwa sababu Mungu anamchukua mbinguni.<br>3. Noa ni mjukuu wa Enoka. Kama yeye, Noa pia anaishi katika ushirika kabisa na Mungu, ni mwenye haki, kwa tofauti na waovu wanaomzunguka.<br>4. Zambi ya watu wa nyakati za Noa inavunja moyo wa Mungu. Anaamua kuwaazibu kwa njia ya garika, lakini anamwokoa Noa.<br>5. Mungu anampa Noa maagizo kwa ajili ya kujenga Safina ili awaokoe katika garika, yeye na familia yake.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| **KUIMARISHA** | Tumia ujuzi! Chora picha ya Noa, familia yake na wanyama ndani ya Safina ikielea juu ya maji. Ita picha yako kwa jina: “Wanaokolewa na Mungu”. | Enoka na Noa ni watu wa aina gani? Ni nini inawatofautisha na watu wengine? |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Mungu anampenda Noa. Anampa namna ya kujitayarisha kwa ajili ya garika na jinsi ya kuendelea kuishi. Mbele, Noa anapaswa kufuata maagizo ya Mungu. Mungu anatuomba tujitayarishe kwa ajili ya hukumu . Anataka kwamba tumwamini Yesu Kristo ambaye alikufa msalabani kwa ajili ya kutuokoa. Umekwisha kumwamini? Uko tayari ili uokolewe? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Soma mara tena daftari ya ma tabia ambayo inapaswa kutofautisha wakristo na dunia, pia ufikiri kuhusu Enoka na Noa, vilevile uhusiano wao na Mungu. Omba Mungu akusaidie kumtumainia na kutembea katika njia zake wiki hii. Unaweza kuchagua tabia ya mukristo mwaminifu na kumwomba Mungu akusaidie kukomea katika ile tabia. |

| | A2 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Noa na garika<br>Kichwa – Anaokolewa na garika | A2 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Noa na garika<br>Kichwa – Kufanya kazi pamoja na Mungu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 8:1-22***<br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 8:1***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anamkumbuka Noa na anamtunza, familia yake na wanyama ndani ya Safina.<br>2. Noa anamshukuru Mungu kwa sababu Mungu alimuokoa katika Safina.<br>3. Mungu anaahidi kwamba hataharibu tena kila kitu kilicho hai. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 5:21-32***<br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 11:5***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anampa Noa maagizo kamili kwa ajili ya kujenga Safina.<br>2. Noa anatii kabisa maaagizo ya Mungu na anaokolewa. |
| KUTANGULIZA | 1. Fanya daftari ya ma namna ambayo familia yako, marafiki zako ao walimu wako wanakutunza.<br>2. Fanya daftari ya ma namna ambayo Mungu anatutunza kila siku.<br>3. Kumbusha kundi umuhimu wa kushukuru familia yetu, marafiki zetu pia walimu wetu juu ya vitu vyote ambavyo wanafanya kwa ajili yetu. Tena ya muhimu zaidi, tunapaswa kumshukuru Mungu ambaye anatuokoa wakati tunamwamini. | Zungumzeni pamoja kuhusu maagizo ya usalama ambayo inapewa ndani ya ndege na vyombo. Watu wanaiheshimu? Kwa sababu ya nini? Kwa nini hapana? Kwa nini tendo la kwamba Noa anatii kila agizo ni kitu cha muhimu sana? |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu hamusahau Noa, familia yake na Wanyama ndani ya Safina. Anatuma upepo duniani na maji ya garika inaanza kushuka.<br>2. Baada ya siku 150 (karibu miezi tano) Safina inasimama juu ya mlima unaoitwa Ararati. Baada ya miezi mbili na nusu, maji inashuka mara tena, na milima ingine inaonekana.<br>3. Baada ya siku makumi ine, Noa anafungua dirisha ya Safina na anaachilia kunguru kwenda, ambaye baada ya kwenda na kurudi mara nyingi, hakurudi tena wakati mwishowe maji inakauka duniani. Kisha Noa anaachilia njiwa kwenda. Njiwa hakute inchi kavu, anarudi kwenye Safina. Baada ya siku saba, Noa anaachilia njiwa kutoka Safina anaenda. Mara hii, wakati anarudi, anachukua jani la mzeituni. Kwa hiyo, Noa anatambua kwamba maji inashuka sana. Wakati anaachilia mara tena njiwa anaenda, baada ya siku saba, harudi tena.<br>4. Mwishowe, miezi kumi na mbili baada ya garika, inchi inakauka tena!<br>5. Mungu anamwambia atoke katika Safina na familia yake na Wanyama.<br>6. Noa anashukuru kweli. Anajenga mazabahu na anamtolea Mungu sadaka.<br>7. Mungu anapendezwa na sadaka ya Noa. Anaahidi kwamba hataharibu tena kila kitu kilicho na uhai.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anamuonya Noa na maelezo yote kuhusu majengo ya chombo kubwa pia kuhusu matayarisho ya garika kubwa ambayo atatuma.<br>2. Mungu anamuonya Noa kwa maelezo yote kuhusu garika.<br>3. Mungu anahaidi kumwokoa Noa, familia yake na Wanyama.<br>4. Mungu analeta maagizo kamili kwa ajili ya kuokoa wanyama. Noa, familia yake na Wanyama wanaingia ndani ya Safina na Mungu anawafungia ndani.<br>5. Garika inafanya siku makumi ine na kila kiumbe kilicho hai ambacho kilikuwa inje ya safina kiliangamia kwa mvua kubwa. Ila tu Noa, familia yake na Wanyama wanaendelea kuishi ndani ya Safina. Mungu anawalinda wote vizuri, kwa sababu wanaelea juu ya maji ya garika.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| KUIMARISHA | Fanya kibao moja na uandike kila kitu ambacho ni sababu ya kumshukuru Mungu, hasa wokovu. | Tunajifunza nini katika historia hii kuhusu tabia ya Noa na ya Mungu? Andika daftari ya maneno ambayo unaweza kutumia kwa ajili ya kutambulisha mtu fulani. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Mungu anamwokoa Noa na anamtunza. Noa anamshukuru Mungu. Mungu anataka na anaweza kutuokoa na kututunza. Tunapaswa kumwamini na kumshukuru. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Soma msatri muhimu. Tutafuata namna gani mfano wa Noa katika maisha yetu?<br>2. Watu ambao weko kandokando yetu wanaweza kufanya nini? |

| | A2 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Noa na garika<br>Kichwa – Mwishowe anatoka katika safina | A2 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Noa na familia yake<br>Kichwa – Kumwabudu Mungu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 9:7-17***<br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 9:15***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anafanya agano na Noa. Anaahidi kwamba hataua tena kwa garika viumbe vyote vinavyoishi duniani.<br>2. Mungu anaweka upinde wa mvua katika mawingu kama kumbukumbu ya ahadi yake. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 8:1-22; 9:11-16***<br>**Mstari muhimu:** ***Waefeso 2:8***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anamkumbuka Noa, familia yake na wanyama.<br>2. Noa anatoa shukrani. Wakati anatoka katika Safina, anamwabudu Mungu kabla ya kufanya chochote kingine.<br>3. Mungu anaahidi kwamba hataua tena wakaaji wa dunia kwa njia ya garika. |
| KUTANGULIZA | Zungumzeni pamoja katika ma kundi za watu wawili kuhusu ma aina tofauti za ahadi ambayo watu wanafanya. Kila mara wanatimiza ahadi zao? | Zungumzeni pamoja katika ma kundi za watu wawili, kuhusu ma barua ya zawadi na ya shukrani. Kwa nini watu wanaituma? Imekwisha kufika kwamba unaituma? Kwa sababu ya nini? |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anamwambia Noa na familia yake wazidi na kujaza dunia.<br>2. Mungu anafanya ahadi ya kipekee, inayoitwa agano, na Noa na watoto wake, pia na Wanyama wote na viumbe vilivyo hai duniani.<br>3. Mungu anaahidi kwamba hataharibu tena dunia na viumbe vyake kwa garika.<br>4. Mungu anaweka upinde wa mvua katika mawingu kwa kukumbuka ahadi yake ya milele, ambayo itadumu kila wakati wote. Hatavunja kamwe ahadi yake.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anampa Noa maagizo yote ili ajenge chombo kubwa na kujitayarisha kwa ajili ya garika ambayo atatuma.<br>2. Mungu anaahidi kumwokoa Noa, familia yake na wanyama, ndani ya Safina kubwa.<br>3. Garika inafika na inadumu siku 40. Ila tu Noa, familia yake na wanyama ndani ya safina, wanaendelea kuishi.<br>4. Garika inamalizika, na polepole maji inashuka. Safina inasimama juu ya mlima Ararati.<br>5. Baada ya siku 40, Noa anaachilia kunguru kutoka katika Safina. Ndege anaendelea Kwenda na kurudi hata maji ilipokauka duniani. Kisha Noa anaachilia njiwa Kwenda. Hapate pahali palipokauka ili asimame, na anarudi kwenye Safina. Baada ya siku saba, Noa anamuachilia kwenda mara tena, asirudi. Inchi iko inakauka.<br>6. Mungu anamwambia Noa aondoke katika Safina na ajizidishe ili ajaze dunia.<br>7. Kitu cha kwanza ambacho Noa anafanya wakati anatoka katika Safina ni kumtolea Mungu sadaka.<br>8. Mungu anafanya agano, ahadi ya kipekee, na Noa, wana wake pia Wanyama wote na viumbe vinavyoishi duniani.<br>9. Mungu anaahidi kwamba hataharibu tena dunia na viumbe vyake kwa garika.<br>10. Mungu anaweka upinde wa mvua katika mawingu kama kumbukumbu ya ahadi yake ya milele, ambayo itadumu wakati wote. Hatavunja kamwe ahadi yake.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| KUIMARISHA | Tumia ujuzi! Fanya kibao moja kuhusu upinde wa mvua. Uipatie jina : “Mungu anatimiza ahadi zake wakati wote!” | Zungumzeni pamoja katika ma kundi kidogo kisha leteni mawazo yenu mbele ya kundi lote: Somo hii inatufundisha nini kuhusu kuabudu? |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Ahadi ambayo Mungu anafanya kwa Noa ni ya milele. Mungu anatimiza ahadi zake wakati wote! Kitu hiki kinapaswa kubadilisha nini katika Maisha yetu? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Noa anamshukuru Mungu. Tunaweza kuonyesha jinsi gani shukrani yetu kwa Mungu kwa ajili ya ma baraka yake kwetu? |

| | A3 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Yesu anamwita Petro | A3 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Petro<br>Kichwa – Mwito wake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 4:17-22***<br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 4:19***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu anaita watu wamfuate.<br>2. Kumfuata Yesu inamaanisha kumwamini, kutubu na kuacha zambi. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 4:17-22; Yoane 1:35-42***<br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 4:19***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Inawezekana kwamba Anderea na Yoane ndio wa kwanza kukutana na Yesu, kisha wanakuwa wanafunzi wake.<br>2. Wanavumbua kwamba Yesu ndiye Masiya na Mwokozi. |
| **KUTANGULIZA** | Eleza kwamba katika michezo nyingi na ma kazi, inabidi ma timu za watu ambao wanafanya kazi pamoja. Yesu eko mwanzo kabisa wa kazi yake na anahitaji watu ambao atafundisha ili waendelee kufanya kazi yake wakati hatakuwapo tena. | Sema kuhusu jinsi watu wengine wanaweza kuwa washabiki wa waimbaji wa pop, washabiki wa timu fulani la mpira, na kazalika. Fasilia kwamba Yesu na maneno yake, vilivuta watu kwake.<br>Eleza pia kwamba Yesu aliita watu wengine ili wawe wanafunzi wake. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Ujumbe ambao Yesu anahubiri ***(Matayo 4:17)***.<br>2. Yesu anaona Petro na Anderea wakitupa nyavu zao.<br>3. Yesu anaita wavuvi, ambao wanafanya kazi kwa bidi na kama timu. Anajua kwamba anaweza kuwafundisha ili watimize kazi yake.<br>4. Utiifu wao wa mara moja kwa mwito wake.<br>5. Yesu anaita pia Yakobo na Yoane. Wao pia wanamtii mara moja. Ndio wanafunzi wa kwanza.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yoane Mbatizaji alisema kwamba Yesu ni Mwana kondoo wa Mungu na Anderea na rafiki yake wanaelewa kwamba Yesu ndiye Masiya ***(Yoane 1:35, 36, 41)***.<br>2. Umuhimu wa tendo la kwamba Anderea anamtambulisha Petro kwa Yesu.<br>3. Kumbe siyo kitu cha kushangaisha jinsi wanamtii Yesu mara moja wakati anawaita wamfuate, baadaye, wakati wanamkuta akihubiri.<br>4. Mfano wa ushuhuda wa Anderea wa kibinafsi.<br>5. Umuhimu wa kumjua Yesu kibinafsi na kumtangaza ku wengine.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| **KUIMARISHA** | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Kwa nini Yesu anaita watu hawa kwa upekee?<br>2. Kutii mwito wa Mungu leo inamaanisha nini?<br>3. Sababu ya nini inaweza kuwa magumu kutii mwito wa Mungu?<br>4. Yesu aliwaahidia nini watu hawa? ***(Angalia Matayo 4:19)*** | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Unajua namna gani kwamba Mungu ana mpango fulani kwa ajili ya maisha yako?<br>2. Yesu ana mpango gani kwa ajili ya wanafunzi wake wa kwanza?<br>3. Kuna faida gani katika kujua mpango wa Mungu.<br>4. Tunaweza kuvumbua namna gani mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha yetu na tunapaswa kujibu jinsi gani? |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Zungumzeni pamoja kuhusu maana ya kutubu leo.<br>2. Andika ombi moja ya kutubu, kisha uiweke katika takataka.<br>3. Fanya utafiti kuhusu mwito wa waamini ambao wanajulikana kabisa leo, kwa mfano, David Livingstone. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Siku hizi tunaweza kumshuhudia Mungu namna gani?<br>2. Fanya daftari ya ma jina na ma cheo za Yesu. |

| | A3 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Uvuvi kubwa | A3 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Petro<br>Kichwa – Changamoto yake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 5:1-11***<br>**Mstari muhimu:** ***Waroma 3:23***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Wanafunzi wanajifunza kumtii Yesu.<br>2. Yesu ni mkubwa na mwenye nguvu na anaweza kufanya miujiza ya ajabu.<br>3. Mungu anaweza kutumia kila mtu anayetubu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 14:22-23***<br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 14:33***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Wanafunzi wanajifunza kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, na anaweza kutuliza woga zetu.<br>2. Imani ndani ya Yesu inatusaidia kushinda zoruba ya maisha. |
| KUTANGULIZA | Sema kuhusu uchunguzi ao mashindano inayofanyika shuleni, kwa ajili ya kuona kama, wanafunzi walijifunza vema vitu ambavyo walifundishwa.<br>Yesu anajaribu Imani na utiifu wa wanafunzi wake muda wa historia ya leo. | Eleza kwamba maisha yetu ni kama safari ambayo inaanza wakati wa kuzaliwa kwetu na inaendelea hata kufa kwetu. Kuna nyakati za utulivu, wakati maisha iko rahisi, na nyakati za zoruba wakati maisha inakuwa magumu. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yesu anasema na watu wengi, akiketi katika chombo cha Petro.<br>2. Wakati Yesu anamaliza kusema, anawaambia wanafunzi waende tena katika uvuvi. (Wamekwisha kufanya uvuvi usiku wote, bila kukamata hata kitu. Wamechoka na wana njaa).<br>3. Petro anafanya kile Yesu anamwambia, na wanakamata samaki nyingi sana.<br>4. Petro anatambua ukubwa wa Yesu na udogo wake ***(Luka 5:8)***.<br>5. Wanafunzi wanaaacha yote ili wamfuate Yesu.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yesu alifanya muujiza kubwa, kisha anatuma wanafunzi ngambo ingine ya ziwa Galilaya.<br>2. Yesu anapanda mlimani kwa kuomba.<br>3. Wanafunzi wanajikuta katika zoruba.<br>4. Yesu anajua, anakuja kwao, akitembea juu ya maji ya ziwa.<br>5. Petro anaomba aende kwake, na anaenda mbele, akitembea juu ya maji.<br>6. Petro anaanza kuzama, anamwita Yesu, na Yesu anamwokoa.<br>7. Fasilia umuhimu wa kumwamini Yesu.<br>8. *Fasilia kwamba wakati tunamwamini Yesu, anaweza kutuokoa katika zoruba ya maisha. Fikirieni kuhusu umuhimu wa kumtumainia Yesu katika nyakati za magumu.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| KUIMARISHA | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Jibu ya Simoni Petro ina maana gani katika ***mstari 5***?<br>2. Tunawezi kujifunza nini katika kukiri zambi yake ***(Mstari 8?)***<br>3. Zungumzeni Pamoja kuhusu maana ya kutubu.<br>4. Jinsi gani tunaweza kuacha yote kwa ajili ya Yesu? | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Namna gani maneno ya Yesu katika ***mstari 27*** inaweza kututia moyo?<br>2. Tunaweza kujifunza nini katika mfano wa Petro katika shairi hii?<br>3. Tunajifunza nini kuhusu kuishi zoruba za maisha? |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Taja ma njia tatu kwa hiyo utamtii Yesu katika wiki inayokuja.<br>2. Ambia mwamini mmoja mwanaume ao mwanamke ambaye unajua aseme kuhusu wakati ambao alitambua usamehe wa Mungu. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Zungumzeni katika kundi kuhusu "zoruba" kubwa ambayo ulipata katika maisha pia fikirieni kuhusu jinsi Yesu anaweza kusaidia katika mambo ya namna hii kwa upekee wakati tunamtumainia.<br>2. Soma ***Isaya 43:2***. Kwa wale wanaomfuata Yesu, ni mapatano gani iko kati ya msatari na sura ambayo tulisoma leo ndani ya Biblia? |

| | A3 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Yesu anamwokoa Petro | A3 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Petro<br>Kichwa – Kukiri kwake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 14:22-33***<br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 14:33***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu ni Mwana wa Mungu.<br>2. Kumwamini Yesu inatusaidia kushinda zoruba za maisha na woga zetu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 16:13-23***<br>**Mstari muhimu:** ***Waroma 10:9***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu “Kristo” ao “Masiya”.<br>2. Jibu la Bwana kwa Petro inaweka msingi wa kanisa. |
| KUTANGULIZA | Zungumzeni kuhusu safari ya maisha. Eleza kwamba maisha yetu ni kama safari ambayo inaanza wakati wa kuzaliwa kwetu na inaendelea hata kufa kwetu. | Moja ya ma swali kubwa ambayo kila mmoja wetu anayo ni hii: Yesu ni nani? Muizungumzie pamoja. Fasilia kwamba watu wa nyakati za Yesu walileta ma jibu tofauti kwa kueleza alikuwa nani, kisha Yesu aliambia wanafunzi wake: “Na ninyi, munawaza kwamba mimi ni nani?”. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yesu anafanya muujiza kubwa, kisha anatuma wanafunzi ngambo ingine ya ziwa Galilaya.<br>2. Yesu anapanda mlimani juu ya kuomba.<br>3. Wanafunzi wanajikuta katika zoruba.<br>4. Yesu anajua, na anakuja kwao, akitembea juu ya maji ya ziwa.<br>5. Petro anaomba Kwenda kwake, na anasonga mbele, akitembea juu ya maji.<br>6. Petro anaanza kuzama, anamwita Yesu, na Yesu anamuokoa.<br>7. *Eleza umuhimu wa kumwamini Yesu.*<br>8. *Eleza kwamba wakati tunamwamini Yesu, anaweza kutusaidia katika zoruba ya maisha.*<br>9. *Fikirini kuhusu umuhimu wa kumwamini Yesu nyakati za magumu.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yesu anajikuta katika mwisho wa kaskazini ya safari yake. *(Onyesha pahali pale katika picha wakati wa majifunzo.)*<br>2. Anauliza: “Watu wanasema kwamba mimi ni nani?” Andika ma jibu ine.<br>3. Kisha, anaaambia wanafunzi wake: “Na ninyi, munasema mimi ni nani?” Angalieni jibu la Petro ya mara moja.<br>4. Kisha, Yesu anafasilia kwamba wale wanaoamini kwamba yeye ni Mwana wa Mungu aliye hai wanatunga Kanisa. Hii siyo jengo lakini kundi la watu waamini.<br>5. Kisha Yesu anatangaza kwamba atakufa na atafufuka toka wafu.<br>6. Petro anajibu kwamba kitu hiki hakitafanyika kamwe. Chunguzeni jibu la Bwana kwa Petro.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| KUIMARISHA | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Yesu anaweza kutusaidia namna gani kushinda woga wetu?<br>2. Taja mambo fulani ambayo inafika zaidi kwa vijana.<br>3. Shairi hii inaweza kusaidia namna gani? | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Tunaweza kuhakikishwa namna gani kwamba sisi ni wa Yesu<br>2. Tunakuwa namna gani memba wa kanisa?<br>3. Ni ma faida gani iko katika kuwa memba wa kanisa? |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Fanya kibao katika ukuta ukiandika mambo katika karatasi ambayo utatia msalabani.<br>2. Chora upinde wa mvua na uandike juu yake moja ya ahadi za Biblia. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Andika kibinafsi maombi kwa kumshukuru Mungu kwa ajili ya Kanisa lake.<br>2. Waza kuhusu mtu ambaye utagawana naye Habari njema ya Yesu. |

| | A3 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Yesu ni nani? | A3 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Petro<br>Kichwa – Katika mlima |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 16:13-23***<br>**Mstari muhimu:** ***Waroma 10:9***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Tunapaswa kushuhudia kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.<br>2. Yesu ndiye mkuu wa kanisa. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matayo 17:1-13***<br>**Mstari muhimu:** ***2 Petro 1:16-18***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu ni wa pekee kama Mwana wa Mungu.<br>2. Yesu ni mkubwa kuliko Musa ao Elia. |
| KUTANGULIZA | Sema kuhusu watu ambao wanajulikana na muchunguze kwa nini wanahesabiwa kama wenye kujulikana sana. Yesu alikuwa mwenye kujulikana kabisa lakini watu wengi hawakujue yeye ni nani kweli. | Sema kuhusu mambo ya kukumbuka ambayo Watoto hawatasahau kamwe. Eleza kwamba wanafunzi hawa tatu hawatasahau kamwe muda ambao walimwona Yesu katika utukufu wake wote mlimani. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yesu anauliza: “Watu wanasema kwamba mimi ni nani?” Andika ma jibu ine.<br>2. Kisha anasema kwa wanafunzi wake: “Na ninyi, munasema mimi ni nani?” Angalieni jibu la Petro ya mara moja. Eleza umuhimu wa kukiri imani kwa Petro na maana yake kwa waamini.<br>3. Kisha, Yesu anafasilia kwamba wale wanaoamini kwamba yeye ni Mwana wa Mungu aliye hai wanatunga Kanisa. *Hii siyo jengo lakini kundi la watu waamini.*<br>4. Kisha Yesu anatangaza kwamba atakufa na atafufuka toka wafu.<br>5. Petro anajibu kwamba kitu hiki hakitafanyika kamwe. Chunguzeni jibu la Bwana kwa Petro.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yesu anachagua watu tatu kati ya wanafunzi wake ili wawe Pamoja naye katika mlima.<br>2. Yesu anaonekana pale katika utukufu wake wote na ukubwa pamoja na Musa na Elia.<br>3. Petro anataka kubaki na kuwafanyia ma hema tatu. Mungu anasema toka mbingu kwa ajili ya kuwakumbusha kwamba Yesu eko juu kabisa kuliko mtu yeyote.<br>4. Wanafunzi wanaogopa lakini Yesu anawafariji na anawafasilia ile inawafikia.<br>5. Onyesha kwamba Yesu ni wa kipekee, na jinsi yeye ni mtu wa ajabu sana.<br>6. *Angalieni jinsi ni ya muhimu kumpa pahali pa kwanza katika maisha yetu.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| KUIMARISHA | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Kwa nini maneno ya Petro ***(Shairi 22)*** ni mbaya sana?<br>2. Kanisa yetu inaweza kutusaidia namna gani kumtumikia mzuri zaidi Mungu?<br>3. Tunaweza kuwa namna gani washuhuda wa kweli ili tuwaambie watu wengine Yesu ni nani kweli? | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Kwa nini ilikuwa ya muhimu kwamba Petro awe mshuhuda wa kugeuzwa kwa Yesu?<br>2. Kwako wewe, wanafunzi walijifunza nini katika hii mambo waliishi?<br>3. Tunaweza kumpa Yesu namna gani pahali pa kwanza katika maisha yetu? |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Fanya kibao katika ukuta ukichora kandokando ya kanisa fulani na uandike ndani ma faida za kuwa memba wa kanisa.<br>2. Chagua mtu moja ambaye unataka kutoa ushuhuda kwake na umuombee mara kwa mara. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Fanya daftari ya vitu ambavyo vinakuzuiza kumtia Yesu pahali pa kwanza.<br>2. ***Shairi 5*** inasema: “Mumsikie”. Chukua muda wiki hii ili usikie ile Mungu anakuambia. |

| | A4 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Mfano wa mapendo | A4 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Mafundisho kwa Petro<br>Kichwa – Unyenyekevu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Yoane 13:1-17***<br>**Mstari muhimu:** ***Yoane 13:15***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu alikuwa mtumishi wa kweli.<br>2. Sisi pia, tunapaswa kutumikia wengine | **Usomaji wa Biblia:** ***Yoane 13:1-17***<br>**Mstari muhimu:** ***Yoane 13:15***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu alikuwa mtumishi mneynyekevu mtiifu ku mapenzi ya Mungu.<br>2. Unyenyenyekevu uko katika msingi wa kazi ya kikristo. |
| KUTANGULIZA | Inchi ambayo Yesu aliishi ni ya joto na kavu. (Uilinganishe na inchi watoto wanaishi. Wakati wa Yesu, watu wana zoezo ya kutembea katika Barabara za vumbi na wakatika wanafika katika nyumba fulani, mwenye nyumbe anafanya kwamba miguu ya wageni wake ioshwe kabla waitwe kwenye chakula (Baadaye munaweza kutaja matendo ingine ya utamaduni inayofanyika kabla ya kuingia nyumbani, katika inchi ya wanafunzi). | Mara nyingi, Bwana Yesu anaeleza ma ukweli ya muhimu ya maisha ya kikristo kwa njia ya mifano yake. Mara hii, anachagua kufundisha kwa matendo yake kwa njia ya iliweza kuitwa “mfano katika matendo”. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Ni siku moja kabla ya kusulubishwa kwa Yesu, na anakula chakula chake cha mwisho pamoja na wanafunzi wake.<br>2. Hakuna mtu ambaye alikumbuka kutimiza utamaduni wa kuosha miguu. Yesu anajitayarisha kuifanya ***(mstari 4-5)***<br>3. Petro anasema kwamba hataki Yesu aoshe miguu yake.<br>4. Yesu anamwambia kwamba anapaswa kuifanya, kama hapana, hana shirika pamoja naye ***(mstari 8)***.<br>5. Yesu anatumia kuosha miguu kwa ajili ya kuonyesha kwamba sisi wote tumechafushwa na zambi na kwa hiyo, sisi wote tunahitaji kusafishwa ao kutakaswa zambi yetu. Yeye pekee anaweza kuifanya kwa sababu alikufa msalabani kwa ajili yetu.<br>6. Yesu anaonyesha pia kwamba tunapaswa kuwa tayari kutimiza ma kazi ya unyenyekevui kwa ajili ya kutumikia wengine<br>7. *Eleza maana ya kujiosha miguu wamoja na wengine.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yesu anasherekea Pasaka pamoja na wanafunzi wake. Wanakumbuka mambo yote ambayo ilifanyika wakati wana wa Israeli waliondoka katika Misri.<br>2. Ni wakati wa chakula hiki Yesu anafundisha kwa njia ya matendo yake mafundisho mbili ya muhimu.<br>3. Mbele ya yote, anachukua pahali pa mtumishi na anasafisha miguu ya wanafunzi wake. Kwa hiyo anawaonyesha kwamba yeye ni tayari kutimiza ma kazi iliyo nyenyekevu kabisa na anawapa mfano wa kufuata (angalia ***mstari muhimu)***.<br>4. Anawaonyesha pia kwamba sisi wote tunahitaji kusafishwa zambi yetu (anatumia mfano wa kuoga, ***mstari 10***). Tunapokuwa wakristo, kila mara tunahitaji kwamba atusafishe miguu siku zote, kwa sababu kila siku, tunatenda zambi na tunahitaji usamehe wake.<br>5. Chunguza mambo ambayo Bwana anamwambia Petro ili usaidie watoto kuelewa habari hii.<br>6. Kisha, anachukua mkate na mvinyo na anaeleza kwamba mkate unamaanisha mwili wake uliosulubishwa na mvinyo, ni damu yake iliyomwangika msalabani. (Angalia ***Luka 22:19-20***).<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| KUIMARISHA | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Zungumzeni pamoja kuhusu nini wakristo wanaweza kufanya kwa ajili ya kutumikiana wamoja na wengine wiki hii.<br>2. Jaribuni tena kuwaza namna gani munaweza kufanya kwa ajili ya kutumikia kundi moja fulani inje ya kanisa, mwaka ujao. | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Zungumzeni pamoja kuhusu namna gani matendo ya unyenyekevu inaweza kufanyika leo.<br>2. Fikirini kuhusu matendo ya namna gani inaweza kutia Mungu pahali pa kwanza katika maisha yetu.<br>3. Fanya majifunzo kuhusu maisha ya mwamini ambaye anajulikana kabisa kwa ajili ya unyenyekevu wake katika utumishi. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Yesu alitumikia wengine namna gani wakati alikuwa katika dunia ?<br>2. Yesu pia alifundisha kwamba hata kama sisi ni wakristo tunaendelea kutenda zambi. Kila siku, tunahitaji kumuomba atusafishe na kusamehe. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Petro anapata mafundisho gani katika sehemu hii ?<br>2. Kusafishwa zambi zetu inamaanisha nini ? Tunapaswa kufanya nini kila siku kwa kubaki karibu na Bwana na kufuata mapenzi yake katika maisha yetu ? |

| | A4 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Alimkana Bwana wake | A4 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Mafundisho kwa Petro<br>Kichwa – Uaminifu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 22:31-34, 54-62***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 22:31-32***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Siyo rahisi kusema kwamba sisi ni wa Yesu.<br>2. Tunapaswa kila mara kujaribu kusema kweli. | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 22:31-34, 39-62***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 22:31-32***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Tunapaswa kuhepuka kujitumainia sisi wenyewe lakini, kumwamini Yesu.<br>2. Tunapaswa kuhuzunika kweli kama tunatenda zambi, kama vile Petro alifanya. |
| KUTANGULIZA | Waza mambo ambamo wanafunzi wanaweza kutafuta kusema uwongo ao kukosa kusema ukweli wote. Muchunguze kwa nini wakati mwingine tunaogopa kusema kweli. Eleza kwamba Petro anajiweka katika hali hii. | Petro alijivuna kwamba hatamuacha kamwe Yesu, kwamba ataenda hata katika kifungo ao kufa kwa ajili yake ***(Luka 22:33)***. Tunajua kwamba kiburi inatangulia kuanguka ***(Mezali 16:18)*** na katika kesi la Petro, kiburi chake inatangulia kuanguka kubaya kabisa. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Petro anafuata kundi ambayo ilimkamata Yesu hata katika nyumba ya kuhani mkuu.<br>2. Anajichanganya na watu walio katika uwanja wa nyumba.<br>3. Wengine wanamuuliza mara tatu kama anamfuata Yesu ao kama ni rafiki yake, anasema uwongo na anajibu kwamba hamujui.<br>4. Yesu anamuangalia Petro, jogoo anawika, na Petro anatambua mambo ambayo anafanya. Anatoka katika uwanja na analia kwa uchungu sana. Anamuacha Yesu wakati ambao Yesu alimuhitaji. Alikuwa na woga na hakuonyesha ujasiri.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Petro anapaswa kuvurugwa. Anajua mambo ambayo Yesu alisema kuhusu kumukana ***(22:34)***. Lakini nPetro anawaza kwamba ni mwenye nguvu na atamsaidia Yesu.<br>2. Wakati wa hatari, anaogopa kusema kweli. Na mwishowe, anamkana Yesu mara tatu, kabisa kama vile Yesu alivyosema kabla.<br>3. Waza kuhusu namna Petro alijisikia wakati anatambua kwamba anamwacha Yesu.<br>4. Zungumzeni Pamoja kuhusu jaribu ya Petro.<br>5. *Zungumzieni pia kuhusu umuhimu wa kuchagua ni wapi tunaenda, tunaenda pamoja na nani na tunawaza nini.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| KUIMARISHA | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Fanya daftari ya ma sababu juu ya ile ni magumu kwetu kuwa wa Yesu, kisha Andika juu yake ahadi moja ya Biblia.<br>2. Petro alimkosea Mungu; hataweza kamwe kupata usamehe wake?<br>3. Vumbua jinsi Daudi alikiri zambi yake na Bati-Seba ***(2 Samweli 11)*** ao ***Zaburi 51*** na namna alirudishwa upya. | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Fanya daftari ya ma hali nzuri ambayo inahitajiwa kwa marafiki wema.<br>2. Taja namna moja kwa hiyo unaweza kuwa mwaminifu kwa Bwana wiki hii.<br>3. Waza kuhusu mambo Yesu alitaka kusema kwa kumuonya Petro kuhusu mambo ambayo inaweza kufanyika. ***(Luka 22:32)***. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Kwa nini wakati mwingine ni magumu kwa waamini kusema kwamba ni wa Yesu.<br>2. Ni nini inatuzuiza kusema kweli? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Tunaweza kuonyesha namna gani kwamba tunahuzunika kweli juu ya zambi yetu?<br>2. Tunaamua namna gani ni marafiki gani ambao tutakuwa nao wakati wote? |

| | A4 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Kifo cha Bwana Yesu | A4 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Mafundisho kwa Petro<br>Kichwa – Mateso na furaha |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Marko 15:22-40***<br>**Mstari muhimu:** ***Wagalatia 2:20***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu ni mkamilifu, bila zambi.<br>2. Tunapaswa kuwa na shukrani kwa sababu ya kifo cha Yesu msalabani kwa ajili yetu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Luka 24:1-12, 33-49***<br>**Mstari muhimu:** ***Luka 24:46-47***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu alipata gazabu ya zambi yetu ili tuokolewe.<br>2. Yesu anatupa usamehe na uzima wa milele. |
| **KUTANGULIZA** | Zungumzeni pamoja kuhusu nini wanafunzi wanaweza kujaribu ikiwa wanakosea mtu kama Petro alivyofanya. Muwaze kuhusu nini Petro angeweza kujaribu kufanya, na kwa nini haikuwezekane. | Eleza kwamba hatujui kabisa Petro anafanya nini wakati Yesu eko msalabani, lakini tunajua kwamba siku ya jumapili ya pasaka, asubui, anaenda kaburini na Biblia inatuambia kwamba siku ile, kweli anakutana na Yesu. (Angalia ***shairi 34.***) |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza jinsi Yesu anapelekwa inje ya mji ili asulubishwe.<br>2. Eleza jinsi anatukanwa na namna wale wanaomzunguka weko wanamzihaki.<br>3. Eleza kwamba ile ma saa tatu ya giza ni kitu cha muujiza na inatusaidia kuelewa kwamba Mungu hakuweza kumwangalia Mwana wake ambaye alikuwa akiazibiwa sababu ya zambi yetu.<br>4. Wakati huu, Yesu alipata azabu ya zambi pahali petu.<br>5. Aleza nini inafanyika wakati Yesu anakufa ***(ma shairi 38-39)***.<br>6. Eleza tendo la akida mbele ya msalaba.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Eleza jinsi wanawake walienda kaburini asubui ya pasaka.<br>2. Eleza ni nini wanakuta kule na ujumbe ambao wanapata.<br>3. Eleza Petro anafanya nini wakati anaposikia Habari hii ***(shairi 12)***.<br>4. Zungumzeni pamoja kuhusu tendo ya kwamba wanafunzi wengine weko na magumu kwa kuamini kwamba Yesu ni hai.<br>5. Eleza nini inafanyika wakati Yesu anawaonekania.<br>6. Petro na marafiki zake wanafurahi kabisa kwa kuona Bwana wao aliyefufuka.<br>7. Yesu anaeleza namna gani mateso yake? ***(ma shairi 45-47)***<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| **KUIMARISHA** | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Muwaze kuhusu maana ya kifo cha Yesu msalabani, kulingana na ***mstari muhimu***, pia kuhusu tendo la kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya kila mtu kwa upekee.<br>2. Zungumzeni pamoja kuhusu ma faida ya kufa kwa Yesu msalabani. Waza ni pahali gani unaweza kuonyesha msalaba juu ya kukumbuka kujitoa kwa Yesu. | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Muwaze namna ya kutenda juu ya kuonyesha kwamba tunahuzunika sababu ya zambi zetu.<br>2. Tunga maneno ya wimbo moja juu ya kusherekea ushindi wa Yesu juu ya kifo, na ufufuko wake. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Kulingana na wewe, kwa nini Yesu alikufa msalabani?<br>2. Tunaweza kuonyesha namna gani shukrani yetu kwa ajili ya kifo cha Yesu msalabani? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Namna gani tunaweza kuwa na uhakika wa kwamba Yesu ni hai?<br>2. Uzima wa milele, maana yake ni nini?<br>3. Tutajua namna gani kwamba tumesamehewa kweli? |

| | A4 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Unanipenda? | A4 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Mafundisho kwa Petro<br>Kichwa – Mapendo |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Yoane 21:1-17***<br>**Mstari muhimu:** ***Yoane 21:17***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Hata wakati tunamkosea Yesu, kama Petro alivyofanya, tunaweza kusamehewa.<br>2. Yesu anapenda kwamba tufundishe watu wengine na tuwachunge kama mchungaji anachunga kondoo zake. | **Usomaji wa Biblia:** ***Yoane 21:1-20***<br>**Mstari muhimu:** ***Yoane 21:15***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Yesu eko tayari kutupa mwanzo mpya.<br>2. Ingawa kushindwa kwetu, siyo kwamba Yesu anatupenda kidogo. |
| KUTANGULIZA | Petro anajaribu kujenga tena maisha yake baada ya kufa kwa Yesu. Anarudi katika jimbo lake la kuzaliwa na anaanza tena kazi yake ya kwanza, ile ya kukamata Samaki katika ziwa la Tiberia. | Bwana Yesu anaonyesha kwamba eko hai, kwa kujionyesha mbele ya wanafunzi wake mara nyingi baada ya kufufuka kwake toka wafu ***(1 Wakorinto 15:3-8)*** |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Wanafunzi wanafanya uvuvi usiku wote lakini na hawakamate kitu. Wanarudi katika pwani wenye kuchoka, wenye njaa na kukata tamaa.<br>2. Bwana Yesu anawaita katika udongo lakini hawamtambui. Anawauliza kama walikamata Samaki.<br>3. Wanatii agizo ya Yesu na wanatupa nyavu yao ngambo ingine ya chombo na wanakamata samaki nyingi sana.<br>4. Yoane anatambua kwamba ni Yesu na Petro anaogelea kwenda kukutana naye.<br>5. Yesu anawaita wote kula pamoja naye, kisha anamuuliza Petro kama anampenda.<br>6. Petro anamjibu kwamba anampenda na Yesu anampa kazi mpya, ya kuchunga wafuasi wa Yesu (kondoo zake).<br>7. Zungumzeni pamoja: Kwa nini Yesu anamuuliza swali moja mara tatu?<br>8. Kumbuka kwamba hakika Bwana alimsamehe Petro kwa sababu anampa kazi ya muhimu sana.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Yesu aliyefufuka anaonekana mara nyingi, kati ya hiyo mbele ya wanafunzi wake 7 ambao walienda kufanya uvuvi katika ziwa la Tiberia.<br>2. Anajitambulisha kwao kwa kuwawezesha kukamata samaki nyingi.<br>3. Wanafunzi wanakula chakula pamoja na Bwana kwenye pwani.<br>4. Bwana Yesu anataka kwamba Petro atubu kwa kweli juu ya mara nyingi ambapo alikosa nyakati za mwisho wa maisha yake.<br>5. Mara tatu, Petro anaonyesha mapendo yake kwa Yesu mbele ya wengine.<br>6. Sasa Petro atakuwa mchungaji ambaye atachunga wale ambao watamfuata Bwana katika Kanisa mpya. Bwana anampa bahati ingine ya kumtumikia.<br>7. *Zungumzeni kuhusu mapendo ya Mungu kwetu; mapendo ya Mungu kwetu haipunguke ingawa makosa yetu, na anatoka tumpende.*<br>8. *Kumbusha wanafunzi kwamba Mungu hawezi kutukosea kamwe hata kama sisi tunamkosea mara kwa mara.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| KUIMARISHA | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Zungumzeni kuhusu jinsi ya kupata wakati wa kumsikia Yesu wiki hii.<br>2. Fanya uchunguzi kuhusu mwamini moja mwenye kujulikana ambaye alijifunza kumsikia Yesu na kufanya mapenzi yake. | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Zungumzeni pamoja namna mapenzdo na usamehe wa Mungu inaweza kututia moyo.<br>2. Fanya uchunguzi kuhusu maisha ya mwamini moja mwenye kujulikana ambaye Yesu alimpa mwanzo mpya. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Tazama namna ni ya muhimu kwetu kuonyesha mapendo yetu kwa Bwana sababu ya mambo yote ambayo alifanya kwa ajili yetu.<br>2. Tambua kwamba Bwana anataka kutupa bahati ingine wakati tunamkosea, na kama tunatubu kweli. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Tutatambua namna gani mapendo ya Mungu kwetu?<br>2. Tutaonyesha namna gani na matendo yetu kwamba Mungu anatupenda? |

| | A5 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Petro anahubiri | A5 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Pentekote |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 2:1-43***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 1:8***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Roho Mtakatifu alipewa kwa wale wanaomfuata Yesu. Ni zawadi.<br>2. Ujumbe ambao ulipewa na wanafunzi ni kwamba tunapaswa kutubu na kuitika usamehe wa Mungu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 2:1-42***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 2:38***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Pentekote ni karamu la wayuda, inasherekewa siku makumi tano baada ya Pasaka.<br>2. Baada ya mahubiri ya Petro, Kanisa ilizaliwa. |
| **KUTANGULIZA** | Muwaze kuhusu namna wanafunzi wanaweza kujisikia ikiwa mabadiliko kubwa inafanyika katika maisha yao. Shule moja mpya, nyumba ingine, mabadiliko ndani ya familia. Eleza kwamba wanafunzi watapata mabadiliko kubwa hivi sasa wanafunzi Yesu anapanda mbinguni, na wanapaswa kuendelea kufanya kazi yake. | Kumbukeni kwamba kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa, ya ndoa, na kazalika, pia karamu za kidini ni vya muhimu katika ma famila zote. Waza kuhusu ma siku kuu katika miezi inayokuja. Taifa la wayuda walikuwa wanasherekea Pentekote siku makumi tano baada ya pasaka, ambayo inakumbusha wakati ambao Waebrania waliondoka katika Misri na ambao Musa alipewa torati katika mlima wa Sinai. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Wanafunzi wanaongojea kuja kwa Roho Mtakatifu ambaye Yesu aliwaahidi ***(Matendo 1:8).***<br>2. Siku ya Pentekote, Roho Mtakatifu alikuja, kama inavyoelezwa katika ma ***shairi 2 na 3***.<br>3. Wanafunzi wanaanza kusema katika lugha zingine ili watu wa ma taifa nyingine ambao wanajikuta katika Yerusalema juu ya karamu, wawaelewe.<br>4. Wengine wanawaza kwamba wanafunzi walikunywa mvinyo nyingi.<br>5. Petro anaanza kusema na anaeleza mbele ya kundi mambo ambayo inafanyika. Anawaambia kwamba unabii wa Yoeli unatimizwa kwa kuja kwa Roho Mtakatifu ***(Yoeli 3:1-5)***.<br>6. Kwa ujasiri, Petro anawaambia kwamba ni wao walimuua Yesu, lakini Mungu alimfufua toka wafu.<br>7. Watu wanavurugwa na wanauliza ni nini wanaweza kufanya.<br>8. Petro anawaambia kwamba watubu na wabatizwe. Siku hiyo hiyo, watu elfu tatu wanaamini na kumfuata Yesu.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Ahadi ya Bwana Yesu inatimilika wakati wanafunzi wanampokea Roho Mtakatifu mu namna ya ajabu siku ya Pentekote.<br>2. Eleza ni nini ilifanyika siku ya kuja kwa Roho Mtakatifu.<br>3. Petro anasema kwamba taifa la wayuda ndio ilimuua yesu, na kwamba Mungu alifufua na kumnyanyua mbinguni na kwamba sasa, anamtuma Roho Mtakatifu.<br>4. Wale wanaamini siku ile wanakuwa wa memba wa kwanza wa Kanisa. Ilizaliwa siku ile na inadumu hata leo.<br>5. Zungumzeni pamoja kuhusu ile iliwafikia kweli wale watu ambao waliamini ***(ma shairi 38 na 39)***.<br>6. Chunguzeni vitu ambavyo wanafanya kwa kuonyesha kwamba maisha yao inabadilika ***(shairi 24)***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| **KUIMARISHA** | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Muwaze kuhusu ukweli wa kwamba Roho Mtakatifu anatupa uwezo ili tushuhudie.<br>2. Zungumzeni pamoja kuhusu umuhimu wa kutangaza Habari njema duniani pote.<br>3. Zungumzeni katika kundi kuhusu jinsi wanafunzi wanaweza kuwa washuhuda muda wa wiki inayofuata.<br>4. Vumbua jinsi toba ilikuwa inafanyika zamani. | **Maswali kwa wanafunzi:**<br>1. Zungumzeni pamoja kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu.<br>2. Zungumzeni kuhusu faida za kukusanyika katika ushirika wamoja na wengine, ndani ya kanisa.<br>3. Tafuta jina la kanisa moja ambayo inaendelea kwa haraka na taja inatambuliwa namna gani. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Kuwa mshuhuda: maana yake ni nini?<br>2. Kutubu: maana yake ni nini? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Kwa nini Pentekote ni ya muhimu kwa Kanisa leo?<br>2. Zungumzeni kuhusu tofauti iliyo kati ya kwenda kanisani na kuwa memba katika kundi la waamini. |

| | A5 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Petro anaponya mgonjwa | A5 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Uponyaji wa mtu kilema |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 3:1-16***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 3:6***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Bwana Yesu ana uwezo wa kuponya maambukizi na magonjwa.<br>2. Anaweza kubadilisha maisha yetu ikiwa tunaweka tumaini letu kwake. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 3:1-26***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 4:10***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anatuweka pahali pazuri na wakati muzuri.<br>2. Ni uwezo wa Mungu ndio ulimponya yule kilema siyo uwezo wa mitume. |
| KUTANGULIZA | Petro na wanafunzi wengine hawatasahau kamwe mfano ambao Yesu aliwafundisha kuhusu Msamaria mwema pia kuhusu lazima ya “kupenda jirani” ***(Luka 10:25-37)***. Mara moja walipomuona mtu huyu mlangoni mwa hekalu, wanajua kwamba wanapaswa kumfanyia kile Yesu angemfanyia. | Kutunza watu wengine ni moja ya vitu vya muhimu sana ambavyo Yesu alifundisha. Mara kwa mara alionyesha kwa wanafunzi wake mapendo yake kwa wote kwa upekee kwa wale walio katika hitaji. Alisema kwamba baada ya Kwenda kwake, wanafunzi watafanya vitu vikubwa zaidi ya vile yeye alifanya. ***(Yoane 14:12)***. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Petro na Yoane wanaenda kuomba katika hekalu.<br>2. Wanakuta mtu mmoja ambaye hajatembea kamwe tangu alipozaliwa, kunapita miaka makumi ine.<br>3. Anawaomba feza, lakini Petro anamjibu kwamba ana kitu kizuri zaidi ya kile; mtu huyu anaweza kuponywa.<br>4. Petro anamsaidia mtu huyu kusimama. Mtu huyu anaanza kuruka na kutembea, na anaingia ndani ya hekalu akisifu Mungu. Ndio muujiza wa kwanza wa kanisa iliyoanzishwa.<br>5. Watu wengi wanakusanyika pale, na Petro anaeleza kwamba mtu huyu hakuponywa kwa nguvu yake yeye, ao kwa nguvu ya Petro, lakini kwa jina la Yesu ambaye watu walisulubisha ***(shairi 16)***.<br>6. Angalia jinsi Imani ya mtu huyu inaelezwa katika ***shairi 16***.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Muda kidogo baada ya Pentekote, Petro na Yoane wanaenda kuomba katika hekalu.<br>2. Wakati wanamuona mtu kilema wanajua kabisa nini Bwana angefanya.<br>3. Kwa Imani, Petro anamsaidia mtu huyu kusimama. Mara moja anaponywa na anaionyesha kwa kutembea, kwa kuruka na kwa kuingia katika hekalu akimsifu Mungu.<br>4. Mara moja aliponywa kabisa; kama vile wakati wa miujiza nyingi ambayo ilitimizwa na Yesu.<br>5. Uwezo wa Yesu unaonekana wazi kupitia mitume wake kwa kuja kwa Roho Mtakatifu.<br>6. Chunguzeni ma nukta kubwa ya mahubiri ya Petro pale anafasilia Yesu ni nani pia vitu ambavyo anaweza kufanya tena.<br>7. Waza kuhusu namna gani Mungu anaweza kupatia wanafunzi wake uwezo wa kuponya.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| KUIMARISHA | 1. Waza kuhusu miujiza ya uponyaji, pia jambo la kwamba wote hawaponywe.<br>2. Zungumzeni kuhusu lazima kwa mkristo wote kutoa ushuhuda kwake (Yerusalema yetu) mbele ya kwenda miisho ya dunia.<br>3. Chunguza maisha ya mkristo moja sasa ambaye aliponyeshwa kwa muujiza.<br>4. Zungumzeni kuhusu mabadiliko ambayo Yesu anaweza kufanya katika maisha yetu wakati tunatia tumaini letu kwake. | 1. Zungumzeni pamoja kuhusu tendo la kwamba kupitiza muda pamoja na Yesu inaweza kusababisha vitu fulani katika ushuhuda wetu na katika kazi yetu ya kila siku.<br>2. Beba wakati kwa kuomba pamoja na wakristo wengine, juu ya kumuomba Mungu amijaze na uwezo, na kuwapatia nafasi kwa kumtumikia.<br>3. Muwaze kuhusu ma sababu juu ya ile Petro alibadilika kweli tangu siku ile alimkana Bwana. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Kulingana na wewe, kwa nini Mungu haponye watu wote?<br>2. Tunaweza kutia tumaini kwa Mungu namna gani siku kwa siku? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Unaweza kujua je kwamba uko pahali ambapo Mungu anataka uwe?<br>2. Tunaweza kumsifu namna gani sisi pia kwa sababu alitusamehe zambi yetu na kubadilisha maisha yetu? |

| | **A5 – KIWANGO 3**<br>**Somo 3 – Maisha ya Petro**<br>**Kichwa – Petro anashuhudia** | **A5 – KIWANGO 4**<br>**Majifunzo 3 – Maisha ya Petro**<br>**Kichwa – Mbele ya baraza** |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 4:1-22***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 4:12***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Roho Mtakatifu alibadilisha kweli maisha ya Petro.<br>2. Wakristo wanapaswa kumtetea Bwana. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 4:1-31***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 4:13***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anampa Petro ujasiri na nguvu ya kushuhudia mbele ya wakubwa wa kidini.<br>2. Wakristo wanapaswa kuwa tayari kwambia wengine habari ya Yesu, mu namna yote. |
| **KUTANGULIZA** | Rudieni mambo ambayo ilitukia katika somo iliyotangulia. Uwakumbushe wanafunzi kwamba katika ma inchi zingine, kumtetea Bwana Yesu inaweza kuleta kama matokeo kuteseka na kufungwa. Katika somo hii, Petro na Yoane wanajikuta katika mateso kutoka kwa wakubwa wa kidini. | Petro alihubiri mahubiri ingine kubwa ***(sura 3)***. Wingi wa waamini unafika karibu 5000 ***(4:4)***. Wakubwa wa kidini walikuwa wanawaza kwamba kusulubishwa kwa Bwana ndiyo mwisho wa wanafunzi wake. Lakini sasa, tazama kwamba wao ni wengi zaidi. |
| **KUFUNDISHA** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Wakubwa wa kidini wanasikia ujumbe wa Petro na wanavurugwa kwa hiyo. Kwa kweli, wanawaza kwamba ni wao tu ndio wanapaswa kufundisha watu, na Petro anahubiri pia kwamba Bwana Yesu ni hai.<br>2. Petro na Yoane wanakamatwa na kuwekwa katika kifungo.<br>3. Siku iliyofuata, wanapaswa kufika mbele ya baraza, mahakama ya kidini, kama vile Yesu alifanya.<br>4. Baraza inataka kujua Petro alitumia uwezo gani ili amutembeshe kilema.<br>5. Petro anawaambia kwamba ni kwa uwezo wa jina la Yesu ***(shairi 10)***.<br>6. Wakubwa wa kidini wanashangaishwa na ujasiri pia uhodari wa Petro na Yoane.<br>7. Wanawaamuru waache kuhubiri kuhusu Yesu.<br>8. Petro anawajibu kwamba lazima kumtii Mungu kuliko wao, watu.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Petro na Yoane wanakamatwa.<br>2. Angalia umuhimu wa baraza (baraza la wayuda).<br>3. Petro anatangaza kwa ujasiri wote mbele ya baraza kwamba ni uwezo wa Yesu ndio ulimponya kilema. Kisha anaeleza kwamba Yesu ndiye Mwokozi pekee yake ***(shairi 12)***.<br>4. Baraza inashangaishwa na ujasiri wa Petro na Yoane, na wanatambua kwamba ni juu walikuwa pamoja na Yesu.<br>5. Baraza inawakataza kuhubiri kwa jina la Yesu. Lakini Petro anawajibu kwamba wanapaswa kumtii Mungu kuliko baraza yenye kutungwa na watu.<br>6. Petro na Yoane wanarudi kwa walio wao na wanaomba pamoja kwamba waweze kuendelea kuhubiri ujumbe kwa ujasiri. Tazameni jinsi maombi yao inapata jibu mu namna ya uwezo.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| **KUIMARISHA** | 1. Fanya muhtasari wa ma nukta za muhimu za imani ya kikristo ambayo inapaswa kuwa msingi wake. Usisahau kwamba Bwana Yesu anapaswa kuwa msingi wa imani ya mwamini. ***(Angalia shairi 12)***.<br>2. Chunguza maisha ya mukristo moja ambaye aliyejulikana vizuri ambaye “alitetea” imani yake, kwa mfano Eric Liddell. | 1. Zungumzeni pamoja kuhusu namna ya kupata bidi nyingi katika imani yenu pia ushuhuda wenu.<br>2. Fanya uchunguzi kuhusu kazi kama majifunzo kwa watu wote kwa ajili ya kujifunza namna wakristo wanaweza kuwa washindaji pahali ambapo kuna mateso. |
| **KUSHIKA** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Ni nini inatuzuiza kuwaambia wengine Habari ya Yesu?<br>2. Kwa mwamini, inamaanisha nini kuwa “jiwe iliyo hai?” ***(1 Petro 2:4-5)*** | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Tutamtumainia namna gani Roho Mtakatifu kwa kutusaidia kushuhudia?<br>2. Namna gani kupingwa kwa Injili inaweza kutusaidia kukomea? |

| | A5 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Petro katika kifungo | A5 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Maisha ya Petro<br>Kichwa – Katika kifungo |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 12:1-19***<br>**Mstari muhimu:** ***1 Yoane 5:14***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mateso inaweza kupata watu wa Mungu.<br>2. Biblia inatufundisha kwamba Mungu anatupenda na anajua ni nini iliyo nzuri kwa ajili yetu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Matendo 12:1-19***<br>**Mstari muhimu:** ***1 Yoane 5:5***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Ni ya muhimu kumtumainia Mungu, kama vile Petro alifanya, hata wakati wa magumu.<br>2. Mungu anaweza kutimiza ile isiyowezekana kwetu, lakini anatuomba kufanya ile inabaki. |
| KUTANGULIZA | Bwana Yesu alisema kwamba, kama vile dunia ilimchukia, ni namna moja dunia itawachukia pia mitume na watu wa Mungu. (Yoane 15:18). Angali mtoto kidogo, Yesu alikuwa karibu kuuawa na mfalme Herode. Sasa mjukuu wa mfalme huyu, ambaye aliitwa pia Herode, eko tayari kutenda namna hiyo hiyo kwa Petro. | Mara tena, Petro anajikuta katika kifungo sababu ya imani yake na mahubiri. Imani yake inapaswa kuwa kubwa, kwa sababu amelala mwenye kufungwa kabisa ndani ya gereza, usiku wa kabla ya kuhukumiwa kwake. Petro amekwisha kujifunza hii ukweli kuhusu ile ataandika baadaye? (1 Petro 5:7) |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mfalme Herode anaamuru kifo cha Yakobo, na wakati anaona kwamba kitu hiki kinapendeza Wayuda, anaamuru kukamatwa kwa Petro.<br>2. Petro anajikuta mara tena katika kifungo, akiongojea kuhukumiwa mbele ya watu wengi.<br>3. Kanisa inakusanyika kwa ajili ya kuomba.<br>4. Usiku uliotangulia kuhukumiwa kwake, malaika anamsaidia Petro kutoka katika gereza.<br>5. Petro anaenda ku nyumba ambapo marafiki zake weko wanaomba.<br>6. Kijakazi ambaye anafungua mlango anawaambia kwamba Petro yupo hapa, lakini hakuna mtu ambaye alimwamini.<br>7. Mwishowe, wanaelewa kwamba Mungu anajibu maombi yao.<br>8. *Muwaze kuhusu umuhimu wa ushirika wa kweli Katikati ya wa waamini.*<br>9. *Muwaze kuhusu jambo hii: Tunapaswa kuomba mara kwa mara, kutarajia kwamba Mungu atatujibu, na kuitika mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yetu.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Kanisa inamjali Petro na inamuombea kwa bidi.<br>2. Petro analindwa na waaskari 16 na anafungwa minyororo mwenye kuambatanishwa na wawili kati ya hawa.<br>3. Malaika moja anatokea, anamuamsha Petro, anamfungua kutoka minyororo yake, na anampeleka inje ya gereza. Hii ni muujiza, Petro eko huru.<br>4. Petro anatambua kwamba ni Bwana ambaye anamfungua.<br>5. Anavumbua kwamba kanisa inaomba lakini bila kutambua kujua kwamba kweli Mungu anaweza kufanya visivyowezekana.<br>6. Inaonekana kwamba Mungu angali na kazi kwa ajili ya Petro. Haijafika bado saa ya kifo chake, sasa Mungu natenda.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| KUIMARISHA | 1. Zungumzeni pamoja kuhusu jambo la kwamba ni magumu kwa wakristo kuomba mara kwa mara.<br>2. Sema kuhusu muda ambao unajua kwamba haukufuate mapenzi ya Mungu.<br>3. Tafuta ma shairi mbili ya biblia kuhusu maagizo ya Mungu kisha muizungumzie pamoja na kundi. | 1. Muwaze kuhusu umuhimu wa kumuomba Mungu mara kwa mara wakati wa magumu.<br>2. Muwaze kuhusu jinsi tunaweza kuomba tukitarajia jibu, na kutia tumaini letu kwa Mungu kwamba atatujibu.<br>3. Ambia rafiki moja ao ndugu akuelezee jinsi Mungu alijibu ombi yao Fulani, kisha zungumzia jibu hii na wengine. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Kwa nini wakati mwingine ma njia za Mungu inaonekana kuwa hazieleweke (wamoja wanaponywa na wengine hapana)?<br>2. Ni namna gani tutavumbua mapenzi ya Mungu juu ya maisha yetu? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Kwa nini mara nyingi tuko na shaka kwamba Mungu atajibu maombi yetu vile tunataka?<br>2. Tunajua namna gani kwamba uwezo wa Mungu ni kubwa kuliko wetu? |

| | A6 – KIWANGO 3<br>Somo 1 – Safari za Abrahamu<br>Kichwa – Tumaini kwa Mungu | A6 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 1 – Abrahamu<br>Kichwa – Mwito wake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 12:1-9***<br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 11:8***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Abramu ni mtu wa imani: anamtumainia Mungu hata kama hajui pahali Mungu atampeleka.<br>2. Wakati Mungu anatuita, kama vile alimwita Abramu, tunapaswa kumtumainia, kumfuata na kumtii. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 11:27-32; 12:1-9***<br>**Mstari muhimu:** ***Matendo 7:2-4***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Abramu ni mtu wa Imani: anamtumainia Mungu hata kama hajui pahali Mungu atampeleka.<br>2. Wakati Mungu anatuita, kama vile alimwita Abramu, tunapaswa kumtumainia, kumfuata na kumtii. Kwa kusema kweli, tunapaswa kutia imani yetu katika mikono yake. |
| KUTANGULIZA | • Uliza wanafunzi wa kundi lako kama kuna siku ambayo walibadilisha shule. Ni magumu gani ambayo inaambatana na hiyo? (Zungumzieni pamoja kuhusu tabia mpya za kushika, njia mpya, marafiki wapya pia walimu wapya ambao watajikuta nao).<br>• Uliza kama ndani ya kundi kuna mtu ambaye amekwisha kuhama. Ni magumu gani ambayo inaambatana na hiyo? Kwa Abrahamu na familia yake, magumu mupya ambayo walipata ni kubadilisha lugha, chakula, hewa pia utamaduni, zaidi ya hii kujikuta mbali na marafiki zao. | Mazungumzo na kutembea. Uliza wanafunzi wa kundi lako kuwaza kama wanaanza safari mrefu kwenda katika inchi ambayo hawajaona kamwe, wakiwa na nia ya kukaa kule. Ni magumu gani ambayo inaweza kupatikana katika hiyo? (Kwa Abrahamu na familia yake, magumu mupya ambayo walipata ni kubadilisha lugha, chakula, hewa pia utamaduni, zaidi ya hii kujikuta mbali na marafiki zao).<br>Andika maneno ifuatayo, kila moja katika karatasi ya muundo wa A4: KUTOKUWA NA UHAKIKA; WASIWASI; JOTO; KUVURUGWA, MAWAZO MENGI. Weka ma karatasi hizi katika ukuta pahali tofauti ndani ya chumba. Ambia vijana watembee wafike pa neno ambayo inaeleza vema ni nini wangesikia katika mambo ya namna hii. Kisha, zungumzieni pamoja kuhusu uchaguzi wao: Kwa nini watajisikia namna hii? |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anasema kwa Abramu na anamwambia aende na familia yake katika inchi ambayo Mungu atamuonyesha. Haitakuwa kitu rahisi. Wakati wa Abramu kusafiri ilikuwa kitu cha magumu na ilikuwa inabeba muda mrefu. Abramu eko pia na vitu nyingi vya kutengeneza pia watu wengi wa Kwenda pamoja naye.<br>2. Mungu, kwa ahadi moja ya upekee, Mungu anjitolea kumbariki Abramu na kufanya familia yake kuwa taifa kubwa. Kupitia hii taifa kubwa, watu wote wa ma taifa mengine watabarikiwa pia.<br>3. Abramu anaenda na mwipwa yake Loti na mke wake Saraï. Wanachukua vitu vyao vyote. Abramu ana umri wa miaka 75!<br>4. Baada ya kusafiri kwa muda fulani, Bwana anamuonekania Abramu pahali panapoitwa Sekemu. Anamwambia Abramu kwamba atatoa inchi hii kwa familia yake.<br>5. Abramu anajenga mazabahu na anamsifu Bwana. Kisha anaenda katika milima kati ya Beteli na Aï na anaweka pale hema yake. Anajenga mazabahu ingine kwa ajili ya kumwabudu Bwana. Toka pale, anaendelea na safari yake Kwenda katika jangwa la kusini.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 1.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anasema kwa Abramu na anamwambia aende na familia yake katika inchi ambayo Mungu atamuonyesha. Haitakuwa kitu rahisi. Wakati wa Abramu kusafiri ilikuwa kitu cha magumu na ilikuwa inabeba muda mrefu. Abramu eko pia na vitu nyingi vya kutengeneza pia watu wengi wa Kwenda pamoja naye.<br>2. Mungu, kwa ahadi moja ya upekee, Mungu anajitolea kumbariki Abramu na kufanya familia yake kuwa taifa kubwa. Kupitia hii taifa kubwa, watu wote wa ma taifa mengine watabarikiwa pia.<br>3. Abramu anaenda na mwipwa yake Loti na mke wake Saraï. Wanachukua vitu vyao vyote. Abramu ana umri wa miaka 75!<br>4. Baada ya kusafiri kwa muda fulani, Bwana anamuonekania Abramu pahali panapoitwa Sekemu. Anamwambia Abramu kwamba atatoa inchi hii kwa familia yake.<br>5. Abramu anajenga mazabahu na anamsifu Bwana. Kisha anaenda katika milima kati ya Beteli na Aï na anaweka pale hema yake. Anajenga mazabahu ingine kwa ajili ya kumwabudu Bwana. Toka pale, anaendelea na safari yake Kwenda katika jangwa la kusini.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 1.** |
| KUIMARISHA | Chora njia ya safari ya Abramu kutoka Karani kufika Beteli na Andika juu ma jina tofauti ya maeneo ambayo imetajwa katika somo hii. Usisahau milima ya Mori pia mazabahu mbili ambayo ilijengwa na Abramu kwa ajili ya kumwabudu Bwana. | Ukitazama historia ya Biblia ambayo tunatoka kujifunza, fanya daftari ya ma tabia ambayo tunaweza kutumia kwa kueleza hali ya Abramu kulingana na mwito wa Mungu wa kumwambia aende katika inchi ingine. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Abramu anamtii Mungu wakati anamwambia aende katika safari, ingawa siyo kitu kilicho rahisi. Ile inatuonyesha nini katika tabia yake?<br>2. Namna gani Imani yetu kwa Mungu inapaswa kuvuta mwenendo wetu siku kwa siku, hata katika mambo ambayo hatuelewi kabisa? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Muwaze katika ma kundi ya watu wawili ao tatu: Abramu anamtii Mungu. Ile inatufundisha nini kuhusu jinsi Abramu anamuona Mungu?<br>2. Muwaze kuhusu mambo fulani ambamo kumtii Mungu inaonekana kuwa magumu. Historia ya Abramu inatufundisha nini kuhusu namna ya mwenendo wetu, hata wakati tunajiona kwamba hatuna na uhakika, tuna wasiwasi, ao tuna Mawazo mengi? |

| | A6 – KIWANGO 3<br>Somo 2 – Safari za Abrahamu<br>Kichwa – Uchaguzi wa kufanya | A6 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 2 – Uchaguzi wake<br>Kichwa – Mwito wake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 13:1-18***<br>**Mstari muhimu:** ***Mezali 3:5-6***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Ni ya muhimu kufanya maamuzi muzuri katika maisha.<br>2. Tunapaswa kumuomba Mungu kutusaidia kufanya maamuzi muzuri. Tunapaswa kumuomba atuongoze. Inapaswa pia kuwaza kumshukuru Mungu na kumwabudu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 13:1-18; 14:1-16***<br>**Mstari muhimu:** ***Yosua 24:15***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Abramu anatafuta msaada wa Mungu na uongozi wake, na anamshukuru kwa hiyo.<br>2. Tunapaswa kumtambua Mungu katika yote tunayofanya, kutafuta msaada wake na maongozi, na kumpa sifa na heshima kwa sababu ya ma baraka ambayo tunapata katika maisha yetu. |
| KUTANGULIZA | • Kila siku tunachagua na tunafanya maamuzi. Uliza kundi ikupe mifano ya maamuzi kidogo ya kila siku na kisha maamuzi kubwa zaidi ambayo inabadilisha maisha. Fanya ma daftari mbili ya hiyo katika kibao.<br>• Leta kwa kila mmoja karatasi. Ngambo moja, wanaweza kuonyesha maamuzi kidogo ambayo walifanya sasa. Ngambo ingine, watachora nini wanatumainia, anatoka ao kutamani kwa ajili ya siku zijazo. Katika ma kundi kidogo wanaweza kuzungumzia Pamoja kuhusu picha zao. Eleza kwamba sisi wote tunapaswa kufanya maamuzi, na tunahitaji kusaidiwa na kuongozwa kwa hiyo. Tunaweza kumtumainia Mungu juu ya kutuongoza vema katika maamuzi yetu na uchaguzi. | Kumtumikia Mungu ni uchaguzi wa kila mtu. Tunaweza kuona tofauti gani katika maisha ya watu ambao wanachagua kumtumikia Mungu? Fanya daftari ya hiyo katika kibao na shika katika akili ma tabia hii muda wa hii majifunzo ya maisha ya Abramu. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Abramu anarudi pahali ambapo aliketi kabla, kati ya Beteli na Aï. Anamjengea Bwana mazabahu, na anaenda kule juu ya kuomba akiita jina la Bwana.<br>2. Abramu eko na uamuzi wa kufanya. Wanakuwa wengi sana kwa kuishi katika eneo lile, na kitu hiki kinasababisha ugomvi. Hakuna nafasi ya kutosha kwa wote, na ni wakati kwa Abramu aachane na mwipwa yake Loti, na aishi pahali pengine mbali naye.<br>3. Abramu anampa Loti nafasi ya kuchagua eneo la inchi ambapo anataka kuishi.<br>4. Loti anachagua uwanja wa Yorodani wenye mboleo, na maji mengi, na anaamua kukaa karibu na miji.<br>5. Abramu anakaa katika inchi ya Kanana.<br>6. Wakati Loti alipoenda, Bwana anasema kwa Abramu na anamuahidia inchi yote ambayo anweza kuona pande zote: kaskazini, kusini, mashariki na mangaribi.<br>7. Mungu anaahidi tena kwa Abramu Watoto wengi na kwamba inchi itakuwa yao.<br>8. Abramu anakaa na kuishi karibu na milima ya Mori, karibu na Heburoni. Anajenga pale mazabahu kwa ajili ya kumwabudu Bwana.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 2.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Abramu eko na uamuzi wa kufanya. Wanakuwa wengi sana kwa kuishi katika eneo lile, na kitu hiki kinasababisha ugomvi. Hakuna nafasi ya kutosha kwa wote, na ni wakati kwa Abramu aachane na mwipwa yake Loti, na aishi pahali pengine mbali naye.<br>2. Abramu anampa Loti nafasi ya kuchagua eneo la inchi ambapo anatoka kuishi.<br>3. Loti anachagua uwanja wa Yorodani wenye mboleo, na maji mengi, na anaamua kukaa karibu na miji.<br>4. Abramu anakaa katika inchi ya Kanana.<br>5. Wakati Loti alipoenda, Bwana anasema kwa Abramu na anamuahidia inchi yote ambayo anaweza kuona pande zote: kaskazini, kusini, mashariki na mangaribi.<br>6. Abramu anakaa na kuishi karibu na milima ya Mori, karibu na Heburoni. Anajenga pale mazabahu kwa ajili ya kumwabudu Bwana.<br>7. Abramu anaishi wakati wa ugomvi. Maadui wa Sodoma, pahali ambapo Loti anaishi, wanashambulia mji na wanamkamata Loti na wanaume wengine, pia wananyanganya mali yao.<br>8. Wakati Abramu aliposikia ile habari, anaenda na jeshi kushambulia na kukomboa wafungwa. Abramu anapiga wanyangani. Hakubali zawadi ya mfalme wa Sodoma, kwa sababu ni Mungu ambaye alimpa ushindi juu ya adui zake.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 2.** |
| KUIMARISHA | Fanya kichwa cha taarifa na muhtasari mfupi wa habari ya kutangaza katika gazeti kuhusu somo yetu ya leo. Katika taharifa hii munapaswa kuwekwa ma nukta kubwa yote ya historia hii. Kazi hii inaweza kufanyika na watu wawili ao katika ma kundi kidogo. Ma taarifa itaelezwa na kuzungumziwa pamoja. | Soma mstari muhimu ***Yosua 24:15***. Kulingana na mafundisho ambayo ulijifunza katika somo hii, Abramu anaonyesha namna gani kwamba yeye ni mtumishi wa Bwana?<br>Rudieni katika daftari ya ma tabia za watumishi wa Mungu ambayo mulifanya hapo katika kutanguliza kwa majifunzo hii. Unataka kuongeza ao kubadilisha kitu fulani? Kumtumikia Bwana inapaswa kufanya tofauti gani katika maisha yetu leo? |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Abramu anamuingiza Bwana katika uchaguzi na maamuzi yake, na Mungu anambariki. Waza kumuomba Mungu akuonyeshe njia na kukuongoza wakati utafanya maamuzi kubwa katika maisha yako. | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Patia kila mmoja karatasi iliyokuwa na maandiko. Uwape wote changamoto ya kupata jinsi ya kumtumikia Bwana katika uaminifu kabisa. Wanaweza kuandika maombi ya upekee ambayo watarudi nayo nyumbani kwa ajili ya kuwakumbusha majifunzo hii. |

| | A6 – KIWANGO 3<br>Somo 3 – Safari za Abrahamu<br>Kichwa – Ahadi za Mungu | A6 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 3 – Abrahamu<br>Kichwa – Tumaini lake |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 11:1-8; 18:1-15; 21:1-5***<br>**Mstari muhimu:** ***Matayo 1:21***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1.Ingawa Abramu alijaribu kutengeneza mambo mu namna yake mwenyewe, Mungu haache mpango wake kwa ajili yake.<br>2. Mungu anahakikisha ahadi yake kwa Abramu, kwamba huyu atakuwa baba wa ma taifa mengi. Ile italeta ma baraka siyo tu kwa Abramu lakini pia kwa watu muda wa historia yote.<br>3. Wakati mwingine tunaweza kuwa na shaka kuhusu ahadi za Mungu kwa sababu zinaonekana kuwa za ajabu kwetu. Pengine tunajaribu kutengeneza vitu sisi wenyewe. Somo hii inatupatia changamoto ya kuamini ahadi za Mungu na kuongojea itimizwe. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 15:1-7; 17:1-19; 18:1-15***<br>**Mstari muhimu:** ***Mwanzo 18:14***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu alimuahidi Abramu mtoto ambaye atakuwa mriti wake. Abramu anamwamini Mungu, lakini yeye na mke wake ni wazee na bado hawajapata mtoto. Wanajaribu kutengeneza vitu wao wenyewe .<br>2. Mungu haache matengenezo yake kwa ajili ya Abrahamu na Saraï. Mungu anahakikisha ahadi yake kwa Abramu, kwamba huyu atakuwa baba wa ma taifa mengi. Ile italeta ma baraka siyo tu kwa Abramu lakini pia kwa watu muda wa historia yote. Wakati mwingine tunaweza kuwa na shaka kuhusu ahadi za Mungu kwa sababu zinaonekana kuwa za ajabu kwetu. Pengine tunajaribu kutengeneza vitu sisi wenyewe. Majifunzo hii inatupatia changamoto ya kuamini ahadi za Mungu na kuongojea itimizwe. |
| KUTANGULIZA | Uliza Watoto kama wamekwisha kufanya ahadi. Kuna mtu ambaye amekwisha kufanya ahadi kwa memba mmoja katika kundi? Andika daftari ya hiyo katika kibao. Wakati mwingine watu hawatimize ahadi zao. Sababu ya nini? (Muizungumzie pamoja). Somo hii inatufundisha kwamba kila mara Mungu anatimiza ahadi zake, hata kama zinaonekana kuwa za ajabu. | Andika katika kibao daftari ya ma ahadi tofauti ambayo watu wanafanya wakati wa sasa (kiapo kya ndoa, kiapo cha kijeshi, makubaliano za kisheria, makubaliano ya malipo, na kazalika). Zungumzieni kuhusu jinsi ahadi hizi zinatimizwa ao hazitimizwe. Majifunzo yetu ya leo inatufundisha kwamba kila mara Mungu anatimiza ahadi zake. |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu aliahidi Abramu watoto wengi.<br>2. Abramu na mke wake Saraï ni wazee na wanajaribu kutengeneza vitu wao wenyewe.<br>3. Lakini mungu hakuache ahadi yake. Kwa kweli anaihakikisha tena kwa Abramu na Saraï. Anawapa jina mpya kama alama ya ahadi hii: Kuanzia sasa wataitwa Abrahamu na Sara.<br>4. Mungu anamwambia Abrahamu kwamba atakuwa baba wa ma taifa mengi. Anaahidi kumpa Abrahamu na uzao wake, na kwamba atakuwa Mungu wao.<br>5. Watu tatu wanakuja kumuona Abrahamu na anawakaribisha kwa wema.<br>6. Bwana anamwambia Abrahamu kwamba sara atapata mwana mwaka ujao. Sara anacheka wakati anasikia habari hii. Yeye na Abrahamu ni wazee kwa kupata mtoto.<br>7. Mungu anatimiza ahadi yake, na Sara anapata kweli mwana.<br>8. Abrahamu na Sara wanaita mwana wao kwa jina la Isaka, maana yake “kucheka”, kwa sababu Bwana anatimiza kwa ajili yao ahadi ya ajabu na anawapa furaha nyingi katika uzee wao.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 3.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu aliahidi Abramu watoto wengi.<br>2. Abramu na mke wake Saraï ni wazee na wanajaribu kutengeneza vitu wao wenyewe.<br>3. Mungu haache ahadi yake kwao. Anahakikisha matengenezo yake. Kuanzia sasa, wataitwa Abrahamu na Sara, kwa kukumbuka ahadi ya Mungu.<br>4. Mungu anamwambia Abrahamu kwamba atakuwa baba wa ma taifa mengi. Anaahidi kumpa Abrahamu na uzao wake, na kwamba atakuwa Mungu wao.<br>5. Watu tatu wanakuja kumuona Abrahamu na anawakaribisha kwa wema.<br>6. Bwana anamwambia Abrahamu kwamba sara atapata mwana mwaka ujao. Sara anacheka wakati anasikia habari hii. Yeye na Abrahamu ni wazee kwa kupata mtoto.<br>7. Mungu anatimiza ahadi yake, na Sara anapata kweli mwana.<br>8. Abrahamu na Sara wanaita mwana wao kwa jina la Isaka, maana yake “kucheka”, kwa sababu Bwana anatimiza kwa ajili yao ahadi ya ajabu na anawapa furaha nyingi katika uzee wao.<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 3.** |
| KUIMARISHA | Soma mstari muhimu, tumia mstari huu kwa kuchora alama moja katika karatasi. Kila mara utakapoiona, waza kwamba Mungu anatimiza ahadi zake, hata kama inaonekana kuwa ya ajabu kwetu. | Katika ma kundi kidogo: Tunajifunza nini ndani ya hii majifunzo kuhusu tabia ya Mungu, ya Abrahamu na Sara? Wanafunzi wataandika Mawazo yao katika karatasi kisha wataizungumzia pamoja ndani ya ma kundi. |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Unamtumainia Mungu?<br>2. Unaami ma ahadi ambayo Mungu anafanya katika Neno lake?<br>3. Namna gani somo hii inaweza kuleta nguvu katika imani yako kwa Mungu? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>1. Katika maisha yako, kuna vitu ambavyo unaona kwamba vina magumu kwa Mungu?<br>2. Unajifunza nini katika majifunzo hii kwa ajili ya kukutia moyo ili umtumainie Mungu katika kila eneo la maisha yako? |

| | A6 – KIWANGO 3<br>Somo 4 – Safari za Abrahamu<br>Kichwa – Mapendo inajaribiwa | A6 – KIWANGO 4<br>Majifunzo 4 – Abrahamu<br>Kichwa – Magumu |
|---|---|---|
| | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 22:1-14***<br>**Mstari muhimu:** ***Yoane 1:29***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anamjaribu Abrahamu. Anamwambia amtoe mwana wake wa pekee. Abrahamu anamtii Mungu na anamtumainia kabisa.<br>2. Ni Mungu anatoa: Analeta zabihu ambayo inachukua pahali pa Isaka.<br>3. Mungu alimtoa Bwana Yesu kwa ajili ya kubeba pahali petu na kufa kama zabihu ili aondoe zambi yetu. | **Usomaji wa Biblia:** ***Mwanzo 22:1-19***<br>**Mstari muhimu:** ***Waebrania 11:17-19***<br><br>**Tunajifunza kwamba:**<br>1. Mungu anamjaribu Abrahamu. Wakati Mungu anamwambia Abrahamu atoe mwana wake, Abrahamu anamtii Mungu na anamtumainia kabisa.<br>2. Ni Mungu anatoa: Analeta zabihu ambayo inachukua pahali pa Isaka.<br>3. Mungu anajua kwamba Abrahamu anamtii, na yeye ni tayari kumpa vyote, sasa Mungu mwenyewe anahakikisha mara tena ahadi zake.<br>4. Mungu alimtoa Bwana Yesu kwa ajili ya kubeba pahali petu na kufa kama zabihu ili aondoe zambi yetu. |
| KUTANGULIZA | Wakati mwingine tunatumia majaribu kwa ajili ya kuvumbua uwezo wa watu fulani. Fanya daftari ya majaribu tofauti ambamo watu wanapaswa kupita (kitambulisho cha ruhusa ya kutembeza gari, mashindano ya shule, mashindano ya mziki, vipimo vya kusikia na kuona, na kazalika). Majaribu hii inaonyesha kiwango chawatu katika ufahamu na uelewa, uwezo wao kimwili ao mwenendo wao. Katika historia hii, Mungu anatumia jaribu moja kwa ajili ya kuvumbua kama Abrahamu anamtumainia kweli. | Kuna kitu fulani ao mtu, katika maisha yako pasipo hicho, ao yeye, hauwezi kuwaza kwamba utaishi? Kwa Abrahamu, mwana wake alikuwa katika kesi hii. Abrahamu aliongojea muda mrefu sana kabla ya kupata mtoto huyu. Abrahamu angejisikia namna gani ikiwa alimpoteza Isaka? |
| KUFUNDISHA | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anamwambia Abramu atoe mwana wake wa pekee Isaka, yule ambaye Mungu alimuahidi. Abrahamu anapaswa kutoa mwana wake kama zabihu (kama sadaka ya kuteketeza katika mazabahu).<br>2. Abrahamu anatii maagizo ya Mungu. Abrahamu anasafiri muda wa siku tatu kwa kufika pahali ambapo Mungu alimwambia aende.<br>3. Wakati Isaka anamuuliza Abrahamu zabihu iko wapi, Abrahamu anajibu kwamba Mungu atajipatia mwenyewe. Ile inaonyesha kwamba Abrahamu anamwamini Mungu kabisa.<br>4. Abrahamu anamtii Mungu kabisa. Yeye ni tayari kuacha yote kwa ajili ya Mungu na kumtoa mwana wake mpendwa.<br>5. Mungu anamwita Abrahamu na anamwambia asimfanye mtoto kitu kibaya.<br>6. Kweli Mungu anajipatia zabihu ambayo itachukua pahali pa Isaka: Kondoo mume.<br>7. Mungu anahakikisha ahadi yake kwa Abrahamu, ya kwamba uzao wake utakuwa wingi na hakuna mtu atakayeweza kuuhesabu. Mungu anaahidi pia kwamba kupitia uzao wake atabariki ma taifa yote duniani.<br>8. *Mungu alituma Mwana wake wa pekee ili achukue pahali petu kama "Mwana kondoo wa Mungu". Kupitia Bwana Yesu, Mungu anatupa baraka ya wokovu, wakati tunaamini na kutia tumaini letu kwake.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Somo 4.** | **Eleza historia ya Biblia.**<br><br>**Zungumzeni pamoja kisha ueleze:**<br>1. Mungu anamwambia Abramu atoe mwana wake wa pekee Isaka, yule ambaye Mungu alimuahidi. Abrahamu anapaswa kutoa mwana wake kama zabihu (kama sadaka ya kuteketeza katika mazabahu).<br>2. Abrahamu anatii maagizo ya Mungu. Abrahamu anasafiri muda wa siku tatu kwa kufika pahali ambapo Mungu alimwambia aende.<br>3. Wakati Isaka anamuuliza Abrahamu zabihu iko wapi, Abrahamu anajibu kwamba Mungu atajipatia mwenyewe. Ile inaonyesha kwamba Abrahamu anamwamini Mungu kabisa.<br>4. Abrahamu anamtii Mungu kabisa. Yeye ni tayari kuacha yote kwa ajili ya Mungu na kumtoa mwana wake mpendwa.<br>5. Mungu anamwita Abrahamu na anamwambia asimfanye mtoto kitu kibaya.<br>6. Kweli Mungu anajipatia zabihu ambayo itachukua pahali pa Isaka: Kondoo mume.<br>7. Mungu anahakikisha ahadi yake kwa Abrahamu, ya kwamba uzao wake utakuwa wingi na hakuna mtu atakayeweza kuuhesabu. Mungu anaahidi pia kwamba kupitia uzao wake atabariki ma taifa yote duniani.<br>8. *Mungu alituma Mwana wake wa pekee ili achukue pahali petu kama "Mwana kondoo wa Mungu". Kupitia Bwana Yesu, Mungu anatupa baraka ya wokovu, wakati tunaamini na kutia tumaini letu kwake.*<br><br>**Eleza mstari muhimu na uwatie wanafunzi moyo ili wajifunze.**<br>**Jaza Majifunzo 4.** |
| KUIMARISHA | Mstari muhimu inatufundisha kwamba Bwana Yesu ndiye zabihu iliyo kamilifu, Mwana kondoo wa Mungu, ambaye anaondosha zambi ya dunia. Unamwamini Mungu na kumuitika Bwana Yesu kama Mwokozi wako? | Abrahamu aliita pahali ambapo mambo ambayo tunajifunza leo ilifanyika kwa jina la: "Yehova-Yire". Mungu atatoa namna gani kwa ajili yetu? |
| KUSHIKA | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Abrahamu anamwamini Mungu kabisa na anamtii, na sababu ya ile Mungu anambariki kwa utele. Tunaweza kufuata namna gani mfano wa Abrahamu? | **Changamoto ya kibinafsi:**<br>Abrahamu anamwamini Mungu na anamtii, hata kama Mungu anajaribu imani yake. Tunaweza kufuata namna gani mfano wake? |

## Mashauri kwa wakufunzi wa masomo

**KIWANGO 3 (Masomo)**
- Wanafunzi watahitaji Biblia kwa kujaza masomo hii. Kwa kweli, watapaswa kutafuta shairi moja ao nyingi.
- Maswali iko na ma namna tofauti, kama mchezo wa maneno, visanduku vya maneno, maneno inayokosekana, na kazalika.
- Masomo imetungwa ili itumiwe na Biblia ya utafsiri wa Swahili ya Congo. Mistari ambayo imetajwa imetoshwa katika utafsiri huu.
- Shabaa ni kwamba, kila mwanafunzi, ingawa Biblia yake, aweze kujibu maswali ya masomo.
- Ma pointi 20 imepewa kwa wiki, na jumla ya ma pointi 80 kwa mwezi, ikiwa majibu yote ni ya kweli.
- Kwa jumla, pointi moja inapewa kwa kila jibu ya kweli, kama ilivyoonyeshwa pembeni ya kila kazi ndani ya kitabu.

**KIWANGO 4 (Majifunzo)**
- Majifunzo hii ina maelezo nyingi kuliko masomo ya kiwango cha 3.
- Ile inaonekana katika maswali magumu na majibu.
- Ma pointi 20 imepewa kwa wiki, na jumla ya ma pointi 80 kwa mwezi, ikiwa majibu yote ni ya kweli na kamili.

**NAMNA GANI KUREKEBISHA MASOMO?**
- Kuangalia kila ukurasa kwa kuchunguza majibu.
- Kuleta ma pointi kulingana na majibu.
- Kutumia kalamu ya rangi tofauti na ile mtoto alitumia.
- Kuongeza, ikiwa ni lazima, jibu inayofaa na kurekebisha makosa ya herufi (lakini hiyo haiwezi kupunguza kiwango cha pointi).
- Kupatia ma pointi kidogo kwa jibu isiyo ya kutosha kabisa ao ya kipande.
- Kuhesabu jumla ya ma pointi kwa mwezi na kuiandika katika ukurasa wa mwisho, pahali palipowekewa.

Ni ya muhimu kuwa mwema katika namna ya kupana ma pointi na kufanya yote iwezekanayo kwa kuwatia moyo watoto katika majifunzo yao ya Biblia. Usisite kusema neno ya kutia moyo, sifa, katika sanduku iliyopangwa kwa hoyo ukiandika kwa mfano rangi ilipakwa mzuri, usafi wa kazi, ma pointi iliyopewa, uelewa muzuri wa somo, na kazalika.
Ni ya muhimu kwa mwanafunzi kuwa mwangalifu kweli ili a tofautishe uchunguzi. Maswali, maoni, misemo ya kutia moyo inaamsha akili ya mtoto. Lakini, kama ni misemo hiyo moja inarudiwa mara kwa mara, kwa wepesi itapoteza bei yake.

**KIWANGO 3**
**Maoni kwa jumla:**
"Kazi nzuri! Inaonekana kwamba ulisoma maswali na usikilivu. Zaidi nilipendezwa na jibu lakoi ku ile ya mwisho; ulifasilia muzuri!"
"Jambo Jonathan. Aksanti kwa kazi yako nzuri. Ni mzuri sana kwa kuwa unapata majibu yote. Nilikamilisha ile ilikosekana."

**Maoni ya kiroho:**
"Musa aliishi mambo magumu na watoto wa Israeli, lakini Mungu hakumwache kushindana nao pekee."
"Yosefu hajasahau kamwe kwamba baba yake alimfundisha kupenda Mungu. Aliikumbuka hata wakati alikuwa mbali na nyumbani."
"Bartimayo aliamua kufika hata kwa Bwana Yesu. Hakukate tamaa, kwa sababu baadaye, aliweza kuona, na alijua kwamba Yesu alikuwa mtu wa kipekee."

**KIWANGO 4**
**Maoni kwa jumla:**
"Mara tena Kazi mzuri sana! Inaonekana kwamba ulielewa vizuri mafundisho hii na ninawaza kwamba ilikupendeza. Aksanti kwa kuchukua muda kwa ajili ya kujibu na utaratibu wote. Ingekuwa raisi kuifanya kwa haraka, nimependezwa na namna yako ya kutumik!"
"Ulifanya nguvu, Rakeli. Nawaza kwamba, kulingana na majibu yako, haukuelewa mambo yote katika mafundisho hii. Pengine unaweza kuisoma mara tena?"
**Maoni ya kiroho:**
"Wakati mwingine imesemwa kwamba mifano ni historia za hapa dunia inayo na maana ya mbingu. Je, unafika kupata maana kamili, ao ya mbingu, ya mfano ulio katika Somo 3?"
"Stefano alipata kifo kibaya, lakini hakuwe na woga wa kufa, kwa sababu alijua kwamba Mungu aliongoza kila kitu, na atakuwa pamoja na Bwana Yesu mbinguni."

© Bible Educational Services 2019

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Congo-Swahili   SWC

07/2024